

**TATHMINI YA ATHARI ZA KIISIMU ZA LUGHA YA KIBOSHO KATIKA  
KUJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA KWA  
WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI**

**MONICA REMI MWACHA**

**TASNIFU INAYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI  
YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA ISIMU (M.A. ISIMU)  
IDARA YA ISIMU NA TAALUMA ZA FASIHI  
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu inayoitwa; **“Tathmini Ya Athari za Lugha ya Kibosho katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili: Mifano kutoka Wanafunzi wa Shule za Msingi”** na kupendekeza ipokelewe na ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa shahada ya Umahiri (M.A Kiswahili).

.....  
Dkt. Zelda Elisifa  
(Msimamizi)

.....  
Tarehe

### **HAKIMILIKI**

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yeyote ile ya Tasnifu hii kwa ajili yoyote kama vile kurudufu nakala na kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria kwa niaba ya mwandishi.

**TAMKO**

Mimi, **Monica Remi Mwacha**, natamka na ninathibitishwa kwamba tasnifu hii inayoitwa: “Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania: Uchunguzi Kifani Wilaya ya Temeke; ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawai kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine kwa ajili ya kutunuku shahada kama hii au nyingine yoyote.

.....

**Sahihi**

.....

**Tarehe**

**TABARUKU**

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa baba, Bw. Remi Paul Mwacha na mama, bi, Elizabeth Peter Mmasy kwa malezi yao bora, upendo wao wa dhati na msaada wao wa hali na mali walionipatia katika maisha yangu ambayo kwa hakika ni hazina kubwa sana kwangu. Mwenyezi Mungu awabariki.

## SHUKURANI

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake, afya njema na kwa namna ya kipekee ninamshukuru kwa zawadi ya uhai aliyonijalia ambayo imenifanya kukamilisha kazi hii.

Pili, ninamshukuru msimamizi wangu Dkt. Zelda Elisifa kwa kujitoa kwake kunisimamia hadi kukamilika kwa utafiti huu. Licha ya kuwa na majukumu mengi lakini alijitotoakwa ajili ya kunisaidia hadi kukamilika kwa kazi hii. Hakika alitoa muda wake na alikuwa tayari kusoma kazi yangu, kuikosoa, kuirekebisha na kunipa ushauri kila ilipobidi bila ya kuchoka wala kukata tamaa. Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na kumzidishia moyo wa upendo ili aendelee kusaidia wengine.

Tatu, ninawashukuru wahadhiri wote wa Chuo Kikuu Huria hususani wale wa Idara ya Kiswahili ambao walinifunza masomo kwa kina na kwa weledi mkubwa. Umahiri na ujuzi wao ndio ulionipa mwanga na ufahamu katika taaluma hii ya isimu na hatimaye kukamilisha kazi hii. Kadhalika, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wote tulioshirikiana wakati wa masomo. Kipekee kabisa ninamshukuru Dotto Biseko aliyetangulia mbele za haki. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Nne, shukurani zangu za dhati zimwendee rafiki yangu mpendwa Amani Senguji Msuya kwa kunitia moyo na kunipa msaada katika kipindi chote nilichokuwa masomoni. Mungu ambariki sana. Aidha, shukrani zangu maalum ziwaendee walenzi wangu wapendwa binamu yangu Willium Ruwaichi Temba na shangazi yangu Agnes Pascal Kimaro kwa malezi yao bora. Pia, ninawashukuru ndugu zangu

Amani, Theresia, Getrudi, Gerumana, Venansi, Cornel, Oscar, Magdalena, Secilia, Aurelia, Victoria, Rosemary Maginga, Innocensia, Lightness, na Wendy kwa upendo, mchango na maombi yao ambayo yamekuwa nguzo iliyonisaidia kutokukata tamaa hadi kufikia mafanikio yangu kimasomo. Shukrani nyingine ziwaendee familia ya Bw. na Bi. Damas Mapunda kwa namna walivyonyonyesha upendo wao wa dhati kwa kipindi chote nilichokuwa masomoni.

Tano, ninamshukuru Mkuu wa Shule ya Sekondari Marangu, Bw. Fedrick Materu kwa kunivumilia kipindi chote nilichokuwa masomoni. Vilevile, ninawashukuru walimu wenzangu Pascal Anselmo na Guido Joseph kwa moyo wao wa kujitolea wakati nikiwa kwenye majukumu ya kitaaluma. Aidha, ninawashukuru watoataarifa wangu wa Shule ya Msingi Masoka, Kirima, Boro na Kidachini kwa utayari wao mkubwa wa kushirikiana nami katika utafiti huu. Hata hivyo, si rahisi kuwataja watoataarifa wote kwa majina ila ninaomba watambue kuwa ninawashukuru sana na Mungu awabariki kwa moyo wa dhati na kwa namna mlivyojitoa na kuacha shughuli zenu ili kukamilisha kazi hii. Nyote nawaambieni ahsanteni sana.

Mwisho, ninatambua kuwa wapo watu wengi ambao ninawiwa kuwashukuru kwa namna walivyonisaidia kipindi chote cha masomo yangu lakini kama sikuwataja, ninaomba radhi. Ninaomba watambue kuwa ninathamini mchango wao ambao menisaidia kukamilisha kazi hii kwa wakati. Mungu awabariki.

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu ni kutathmini “*Athari ya Lugha ya Kibosho katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili: Kwa Kutumia Mifano kutoka kwa wanafunzi wa shule za msingi*”. Malengo mahususi matatu ya utafiti ni; kwanza ni kubaini athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi, pili lilikuwa ni kutathmini sababu zinazo wasababisha wanafunzi wa Kibosho kama L1 kuathiriwa na lugha yao katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 na tatu ni kuainisha mbinu za kipedagogia katika kusahihisha athari za wanafunzi wanaozunguma Kibosho kama L1 wakati wanajifunza Kiswahili kama L2. Nadharia iliyoongoza utafiti huu Uchanganuzi Linganuzi (UL) ambayo huchunguza athari ya L1 kwenye L2. Mbinu mbalimbali za utafiti zilitumika; pia data zilikusanywa katika Wilaya ya Moshi Vijijini katika shule za msingi za Masako, Boro, Kidachini na Kirima Juu. Watoa taarifa waliohusika ni wanafunzi na walimu wa shule hizo. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu; hojaji, mahojiano na mbinu ya insha. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa lugha ya Kibosho imeathiri lugha ya Kiswahili hususani katika vipengele vya kimatamshi, kimsamiati na kimaana. Pia yameonesha kuwa kuna sababu mbalimbali zilizochangia lugha ya Kiswahili kuathiriwa kama vile; uzoefu wa kutumia lugha mama na athari za matamshi katika lugha ya Kibosho. pia, mbinu za kipedagogia za kusahihisha athari hizo ni pamoja na walimu wawaelekeze wanafunzi utamkaji mzuri wa matamshi na yaandaliwe makongamano, warsha na mafunzo mbalimbali kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unapendekeza watafiti wajao wafanyie utafiti juu ya athari za kimuundo za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.



## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO .....</b>	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TAMKO .....</b>	<b>iv</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>v</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>vi</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>viii</b>
<b>YALIYOMO.....</b>	<b>ix</b>
<b>ORODHA YA MAJEDWALI .....</b>	<b>xii</b>
<b>ORODHA YA VIELELEZO .....</b>	<b>xiii</b>
<b>ORODHA YA FINYAZO NA VIFUPISHO .....</b>	<b>xiv</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI WA JUMLA.....</b>	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	5
1.3 Malengo ya Utafiti .....	5
1.3.1 Lengo Kuu .....	6
1.3.2 Malengo Mahususi .....	6
1.3.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.4 Umuhimu wa Utafiti .....	6
1.5 Mawanda ya Utafiti.....	7
1.6 Mpangilio wa Tasnifu .....	7
1.7 Hitimisho la Sura ya Kwanza.....	8

<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>9</b>
2.1 Utangulizi.....	9
2.2 Athari ya Lugha ya Kwanza katika Uamiliaji wa Lugha ya Pili .....	9
2.3 Pengo la Utafiti .....	16
2.5 Hitimisho la Sura ya Pili .....	19
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>20</b>
<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>20</b>
3.1 Utangulizi.....	20
3.2 Usanifu wa Utafiti.....	20
3.3 Eneo la Utafiti .....	20
3.4 Sampuli ya Utafiti .....	21
3.5 Usampulishaji .....	22
3.6 Mbinu za Kukusanyia Data.....	23
3.6.1 Mbinu ya Dodoso.....	24
3.6.2 Usaili .....	24
3.6.3 Mbinu ya Insha .....	25
3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data.....	26
3.8 Mkabala wa Utafiti.....	26
3.9 Itikeli ya Utafiti.....	27
3.10 Hitimisho la Sura ya Tatu .....	28
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>29</b>
4.1 Utangulizi.....	29
4.2 Athari ya Lugha ya Kibosho Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.....	29
5.1 Utangulizi.....	51

5.2	Muhtasari wa Utafiti .....	51
5.2.1	Mchango wa Utafiti .....	53
5.3	Hitimisho la Utafiti .....	54
5.4	Mapendekezo ya Utafiti .....	54
	<b>MAREJELEO .....</b>	<b>56</b>
	<b>VIAMBATANISHO .....</b>	<b>60</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Mtawanyiko wa Sampuli ya Watafitiwa .....	22
Jedwali 4.1: Athari Chanya za Lugha ya Kibosho Wakati wa Kujifunza Kiswahili .....	31
Jedwali 4.2: Athari Katika Matumizi ya /S/ badala ya /Z/ .....	33
Jedwali 4.3: Athari katika Matumizi ya /dh/ .....	36
Jedwali 4.4: Athari katika Matumizi ya Sauti /f/ badala ya /v/ .....	37
Jedwali 4.5: Athari katika Matumizi ya Sauti /S/ badala ya /th/ .....	40
Jedwali 4.6: Athari za Kimaana wakati wa Utamkaji wa Maneno .....	41
Jedwali 4.7: Athari za Kimatamshi .....	43

## **ORODHA YA VIELELEZO**

Kielelezo 4.1: Insha Iliyoandikwa na Mwanafunzi wa Darasa la Saba .....	34
Kielelezo 4.2: Insha Iliyoandikwa na Mwanafunzi wa Darasa La Saba .....	38

**ORODHA YA FINYAZO NA VIFUPISHO**

/ /	Mipaka ya Fonimu
Bi.	Bibi
Bw.	Bwana
Kb	Kibosho
L1	Lugha ya Kwanza
L2	Lugha ya Pili
MLUTA	Mradi wa Lugha Tanzania
UL	Uchanganuzi Linganuzi

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI WA JUMLA**

#### **1.1 Usuli wa Mada**

Wataalamu mbalimbali wanakubaliana kuwa lugha ni sehemu muhimu sana katika maisha ya binadamu na katika jamii wanamoishi. Hivyo, palipo na watu huwepo pia na lugha (Obuchu na Mukhwana (2015). Mtoto anapozaliwa hujifunza lugha ambayo inatumiwa na watu wanaomzunguka hususani nyumbani. Lugha hii ambayo mtoto anapozaliwa hujifunza kwa mara ya kwanza huitwa lugha ya kwanza (L1). Lugha ya kwanza kwa wataanzania walio wengi huhusisha lugha za kijamii ambazo hutambulikana pia kama lugha za makabila kwa sababu hubeba jina la kabila husika. Mathalani, kuna lugha kama Kibosho ambayo huzungumzwa na watu wa Kibosho, Kisukuma kinachozungumzwa na Wasukuma na Kimeru kinachozungumza zaidi na Wameru. Ingawa maelezo ya wataalamu wengi yanaonesha kuwa lugha za makabila nyingi ndizo zinazoweza kuwa lugha ya kwanza lakini Kiswahili pia kinaweza kuwa lugha ya kwanza kwa baadhi ya watu hususani wale waliozaliwa maeneo yenye lugha mchanganyiko ambapo lugha ya mawasiliano ni Kiswahili pamoja na wale waliozaliwa na wazazi wenye makabila tofauti ambapo lugha yao ya mawasiliano ni Kiswahili.

Baada ya mtoto kufikia umri fulani ambao humwezesha kuchangamana na watu zaidi hususani katika mfumo rasmi wa elimu, hujifunza lugha ya pili. Kwa hiyo, lugha ya pili (L2) ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Lugha hii inaweza kuwa ya asili ya jamii ambamo mtu anaishi au ya kigeni. ugha hii hukusudiwa kumwezesha mzungumzaji kuwa na wigo mpana wa

mawasiliano katika jamii. Mtu hujifunza lugha ya pili kwa madhumuni mbalimbali ikiwamo kupata elimu, taarifa au kuwasiliana na watu wanaotumia lugha hiyo. Lugha ya pili mara nyingi mtu hujifunza katika mazingira rasmi kama shuleni au wakati mwingine katika mazingira yasiyo rasmi kama kwa wanajamii wanaozungumza. Kwa hiyo, mjifunzaji anaweza kukumbana na changamoto mbalimbali za ujifunzaji. Changamoto hizo zinaweza kutokea kwa sababu mjifunzaji huwa anafahamu lugha ya kwanza ambayo imejengeka akilini mwake. Hivyo, upo uwezekano wa kuathiriwa na lugha ya kwanza wakati wa kujifunza lugha ya pili kwa sababu lugha zinatofautiana kisarufi.

Akiafanua zaidi kuhusu dosari wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili, Lado (1957) anaeleza kuwa dosari za wazungumzaji wa lugha ya pili zinasababishwa na mwingiliano wa lugha ya kwanza. Maelezo haya yanamaanisha kuwa dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili husababishwa na mwingiliano wa lugha ya kwanza na pili. Kwa upande wake Corder (1967), naye anadai kuwa dosari katika lugha ya pili yanaonyesha hali fulani ya matatizo aliyonayo mzungumzaji wa lugha ya pili kutokana na kuhamisha sifa fulani za lugha ya kwanza hadi kwenye lugha ya pili.

Kwa upande wao Fromkin na wenzie (2007), wanadai kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili hutegemea mfumo wa kisarufi wa lugha yao ya kwanza. Baadhi ya makosa yanajitokeza wakati wahusika hao wanapojifunza lugha ya pili hujikita katika uhamishaji wa kaida za kisarufi za lugha ya kwanza. Wataalamu hawa wanaendelea kuelezea kuwa athari ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili hudhihirika zaidi katika fonolojia, mofolojia na sintaksia.



Maelezo ya Lado, Corder na Fromkin yanaonesha kuwa dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili yanasababishwa na kuwapo kwa mwingiliano wa lugha ya kwanza na ya pili. Hii ni kwa sababu mjifunzaji wa lugha ya pili kuhamisha sifa za lugha ya kwanza na kuzitumia katika lugha ya pili. Kwa kuwa lugha hutofautiana kitabia (sarufi) upo uwezekano wa kutumia sarufi ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili hali ambayo husababisha dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu namna lugha ya kwanza inavyoathiri lugha ya pili katika uamiliaji wa lugha. Kwa mfano, Mangwa (2005) alichunguza athari za Kikisii katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili na kubaini kuwa athari za tahajia, sarufi na msamiati za Kikisii zinajitokeza katika lugha ya Kiswahili. Joy (2012) alifanya utafiti kuhusu dosari za kisintaksia zilizofanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiidakho waishio Kenya. Alibaini matumizi yasiyosahihi ya viambishi awali vinavyowakilisha mtenda, matumizi yasiyo sahihi ya viambishi vinavyobeba dhana ya ukubwa, udogo na vimahali.

Naye Nyanda (2015) alitafiti athari ya lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili na kubaini athari zinazopatikana katika matamshi, msamiati na maana kwa ujumla. Naye Wenceslaus (2015) alitafiti athari za kifonolojia ya lugha ya Kijita katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili alibaini athari hizo hujitokeza katika nyanja ya matamshi na maumbo mathalani uchanganyaji wa sauti wa kuzungumza na kuongeza viambishi vya maneno pasipostahili. Kwa upande mwingine Mpangala (2018), alichunguza athari za lugha ya Kimakonde katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na katika utafiti wake alibaini

watoto wa Kimakonde wanapojifunza lugha ya Kiswahili huathiriwa na lugha ya Kimakonde katika matamshi, upandishaji na ushushaji wa sauti sehemu isiyohusika, uchanganyaji wa sauti wakati wa kuzungumza, kuvuta sauti wakati wa kuzungumza pamoja na kuweka mkazo pasipohitajika.

Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu wengi yanaonesha kuwa katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya pili kuna mwingiliano wa maarifa ya awali kutoka lugha ya kwanza. Hali hii huchangiwa zaidi na lugha ambazo zinashabihiana kiisimu. Lugha ya Kiswahili ambayo ni moja ya lugha za Kibantu ni lugha ya pili kwa watumiaji wengi wanaozungumza Kiswahili. Kama ilivyoelezwa awali kuwa lugha hii ya Kiswahili mwanafunzi hujifunza katika mfumo rasmi wa elimu huku akiwa tayari ana lugha yake ya asili ambayo mara nyingi ni ya Kibantu. Kutokana na ukaribu wa lugha hizo ambazo hutoka katika mbari moja, upo uwezekano wa lugha ya kwanza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili katika vipengele mbalimbali vya sarufi kama ambavyo tafiti tulizozijadili zinavyoonesha.

Kibosho ni lugha mojawapo ya lugha za Kibantu na ambayo ni lugha ya kwanza kwa wazungumzaji wa Kibosho huku Kiswahili kikiwa ni lugha yao ya pili. Katika mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili inaonekana kuwa kuna athari zinazojitokeza. Hata hivyo, suala hili bado halipo bayana kwa kuwa lugha zinatofautiana kitabia. Hivyo, mahitimisho yaliyotolewa katika tafiti zingine kama Kisukuma, Kinyamwezi na Kikisii hayawezi kutumiwa kuelezea athari za Kibosho katika Kiswahili. Hivyo, ipo haja ya kuchunguza suala hili kimahususi zaidi. Kwa hiyo, utafiti huu utafiti huu ulifanyika ili kutathmini athari ya lugha ya Kibosho kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule teule za msingi.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Tafiti nyingi zinaonesha kwamba katika mchakato wa ujifunzaji lugha ya pili, lugha ya kwanza huathiri lugha hiyo katika vipengele mbalimbali (Wenceslaus, 2015; Mpangala, 2018). Imeelezwa kuwa tafiti nyingi zinaonesha kwamba lugha za asili huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili kwa sababu mzungumzaji wa lugha ya kwanza ana maarifa ya lugha yake ya kwanza. Hivyo, huweza kuyatumia maarifa hayo katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hali hii huweza kusababisha dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kuwa lugha hutofautiana kitabia. Kibosho ni moja ya lugha za asili ambayo ni lugha ya kwanza kwa wazungumzaji wengi wa eneo la Kibosho.

Baada ya lugha hii, wazungumzaji hulazimika kujifunza lugha ya pili ambayo kwa wengi wao ni Kiswahili wakiwa katika mfumo rasmi au si rasmi. Kama ilivyoelezwa kuwa lugha za asili huweza kuathiri lugha ya pili wakati wa ujifunzaji. Hata hivyo, suala hili bado halipo bayana kwa kuwa haifahamiki athari za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili ni zipi. Ingawa zipo tafiti kadhaa zilizotafiti athari za lugha za asili katika ujifunzaji wa Kiswahili lakini lugha zinatofautia kitabia. Hivyo, hitimisho la lugha fulani haliwezi kuwa hitimisho la lugha zote. Kwa hiyo, ipo haja ya kutafiti zaidi suala hili katika lugha mahususi. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

## **1.3 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu una malengo ya aina mbili: lengo kuu na malengo mahususi.

### **1.3.1 Lengo Kuu**

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi za Kibosho.

### **1.3.2 Malengo Mahususi**

- i. Kubainisha athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi za Kibosho.
- ii. Kutathmini sababu za athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.
- iii. Kuainisha mbinu za kipedagogia katika kusahihisha athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika Ujifunzaji wa Kiswahili.

### **1.3.3 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu ulijibu maswali mahususi matatu kama ifuatavyo:

- i. Kuna athari zipi za kiisimu za lugha ya Kibosho zinazojitokeza kwa wanafunzi wa shule za msingi za Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili?
- ii. Zipi ni sababu za athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kibosho?
- iii. Mbinu gani za kipedagogia zitumike katika kusahihisha athari za kiisimu katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili?

### **1.4 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utasaidia kuongeza maarifa katika uwanja wa isimu husuani katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti huu unatarajiwa kuongeza maarifa kuhusu athari

za Kibosho zilizojitokeza katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Maarifa hayo yatasaidia kubaini kiwango cha athari ya Kibosho katika kujifunza Kiswahili pamoja na kubainisha mbinu za kuondoa athari hizo ili kuepuka dosari zinazoweza kutokea. Pamoja na hayo, kukamilika kwa utafiti huu kutakuwa ni chachu kwa watafiti wajao kutafiti zaidi kuhusu suala la athari za lugha mbalimbali katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Uchunguzi wa athari hizo utasaidia kujua na kuyarekebisha makosa mbalimbali yanayosababishwa na lugha ya kwanza.

### **1.5 Mawanda ya Utafiti**

Utafiti huu umetathmini athari ya lugha ya Kibosho kama L1 katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2. Athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili zinaweza kuwa za msamiati, miundo, maumbo na maana. Lakini utafiti huu ulijikita kuchunguza vipengele vya matamshi, msamiati na maana kati ya vipengele vingi vinavyoweza kuchunguzwa. Uteuzi wa vipengele hivyo ulitokana na maelezo ya tafiti nyingi za awali ambazo zilibainisha kuwa athari nyingi zilijidhihirisha katika vipengele hivyo. Utafiti huu haukushughulikia kipengele cha kimuundo cha lugha ya Kibosho kilivyoathiri lugha ya Kiswahili. Kwa upande wa mawanda ya utafiti huu kijiografia, utafiti huu ulifanyika katika shule za msingi tu zilizopo kata ya Kirima wilaya ya Moshi vijijini mkoani Kilimanjaro.

### **1.6 Mpangilio wa Tasnifu**

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya Kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa tasnifu. Sura ya Pili inahusu mapitio ya maandiko pamoja na kufafanua nadharia uliyoongoza utafiti huu. Sura ya Tatu imebainisha mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu. Sura ya Nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data na Sura

ya Tano inahusu muhtasari wa utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti. Kipengele kinachofuata kinatoa hitimisho la sura ya kwanza.

### **1.7 Hitimisho la Sura ya Kwanza**

Sura hii imetoa utangulizi wa jumla kuhusu vipengele muhimu vya kiutangulizi. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na mawanda ya utafiti. Sura inayofuata inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kubainisha kiunzi cha kinadharia.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii imefafanua vipengele viwili ambavyo ni mapitio na kiunzi cha nadharia. Sehemu ya kwanza inafafanua mapitio ya maandiko mbalimbali yaliyohusiana na mada ya utafiti huu. Katika ufafanuzi huo, tumefafanua kile kilichofanywa na watafiti tangulizi kisha kubainisha pengo la utafiti lililokusudiwa kuzibwa na utafiti huu. Sehemu ya pili ya sura hii tumefafanua kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu.

#### **2.2 Athari ya Lugha ya Kwanza katika Umiliaji wa Lugha ya Pili**

Lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtu hujifunza mara tu azaliwapo. Mtoto hujifunza zaidi lugha hii kutoka kwa wanaomzunguka. Lugha ya pili kwa kawaida mtu hujifunza kutoka kwa wanajamii na zaidi kutoka katika mfumo rasmi wa elimu. Mhalani, kwa Tanzania, lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumiwa sana kama lugha ya pili. Hii ni kwa sababu watu wengi lugha zao za kwanza ni za makabila. Hivyo, wanapozaliwa huanza kuzungumza lugha hiyo kisha kujifunza Kiswahili katika jamii au katika muktadha rasmi, yaani shuleni. Hata hivyo, wapo baadhi ya watu ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili na lugha ya pili kuwa lugha nyingine ya asili au ya kigeni.

Katika mchakato wa ujifunzaji hususani lugha ya pili, kuna mwingiliano unaojitokeza na lugha ya kwanza hasa kwa kuwa mjifunzaji hujifunza L2 tayari akiwa na kanuni za L1. Kwa hiyo si ajabu ikatokea kuchanganya baadhi ya maelezo ya L1 katika kujifunza L2. Hii inadhihirishwa na baadhi ya tafiti zilizochunguza

athari za L1 katika ujifunzaji wa L2, kama ilivyofafanuliwa hapa chini, Massamba (1986) katika kuchunguza athari za lugha mama katika Kiswahili mkoani Mara aligundua kuwa, lugha za asili na lugha ya Kiswahili ziliathiriana. Mtaalamu huyu, alichunguza jinsi lugha za asili zilivyoathiri Kiswahili kifonolojia, kimsamiati na kisarufi. Katika fonolojia, Massamba anaonyesha jinsi sauti zilivyoongezwa au kudondoshwa katika matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha ya kwanza, hali iliyosababisha dosari ya utamkaji.

Kuhusu msamiati, Massamba anaelezea kuwa baadhi ya maneno kutoka lugha ya kwanza za watu wa Mara, yalipenyezwa na kutumiwa katika Kiswahili sanifu. Matokeo ya matumizi haya ni kuvuruga usanifu wa Kiswahili ambacho tayari kilikuwa na misamiati mwafaka wa kurejelea vitu au hali husika. Kwa upande wa sarufi, viambishi vinavyohamisishwa kutoka lugha za kwanza na kuingizwa katika Kiswahili vilisababisha makosa ya kimofolojia na yale ya kimuundo. Hali hii, kwa maoni ya mtaalamu huyu, ilikiuka kaida za Kiswahili sanifu na hivyo kutatiza uwasilishaji wa ujumbe.

Bosha (1993) alichunguza athari za Kiarabu katika Kiswahili. Alijikita katika ukopaji wa maneno kutoka katika Kiarabu yaliyotumiwa katika Kiswahili. Mtafiti huyu aligundua 44.3% ya maneno yanayotumiwa katika Kiswahili chanzo chake ni Kiarabu. Anaendelea kuelezea kwamba hali hiyo haifanyi lugha ya Kiswahili kuchukuliwa kuwa ni Kiarabu, lahaja ya Kiarabu wala pijini ya Kiarabu. Mtaalamu huyu alisisitiza kwamba hakuna lugha ambayo inaweza kukua kipweke kama kisiwa bila kuathiriwa wala kuathiri lugha nyingine.



Bartoo (2004) alichunguza kuhusu ujifunzaji wa sintaksia ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaotumia Kikeiyo kama lugha ya kwanza. Mtafiti huyu aligundua kuwa Kikeiyo kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiingereza. Anasema kwamba, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizo mbili, wanafunzi husika walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao hadi kuwa katika lugha ya Kiingereza. Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyobainisha mtafiti huyu katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafiti wa hao. Vilevile, Ngugi (2007) alichunguza athari ya fonolojia ya lugha ya Kikuyu (L1) katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2). Katika kuchunguza namna lugha ya Kikuyu ilivyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, mtafiti huyu aligundua kuwa athari zilijitokeza katika matamshi na tahajia. Amesisitiza kwamba makosa mengi yanajitokeza katika matumizi ya lugha ya wanafunzi wa shule za upili waliotumiwa kama watafitiwa yalitokana na uchopekaji, udondoshaji na unazalishaji.

Mifanyiko hiyo ya kifonolojia ilidhihirika katika matumizi ya lugha ya wanafunzi husika huku makosa yakijitokeza kutokana na tofauti katika lugha. Kwa mfano, uchopekaji huo ulihusu sauti nazali /n/ na /m/. Mathalani, neno “*umewandia*” badala ya “*umewadia*” lilidhihirisha uchopekaji huo wa sauti /n/. Akiongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa, alisahihisha insha 285 na kubainisha kuwa maneno 424 hayakuendelezwa ipasavyo. Makosa hayo aliyahusisha na athari ya fonolojia ya L1.

Utafiti wa Ngugi unakaribiana na ule wa Ng’ang’a (2002) ambaye alifanya utafiti kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wa jamii ya Wakikuyu waliokuwa wanajifunza Kiingereza kama L2. Utafiti huo ulihusisha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa darasa la saba na jinsi zilivyoshughulikiwa na walimu katika

tarafa ya Ndaragwa nchini Kenya. Uchunguzi huo, ulishughulikia dosari za kisintaksia, kisemantiki, kimofolojia na kitahajia. Hata hivyo, ilibainika kwamba dosari hizo zilisababishwa na athari za L1. Kama Ngugi, Ng'ang'a aligundua kwamba, lugha ya Kiingereza (L2) iliathiriwa na lugha ya Kikikuyu kwani makosa mengi yaliyobainishwa yalitokana na L1. Tafiti za Ngugi na Ng'ang'a zimetusaidia kubaini athari za kimofolojia na kifonolojia katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kwa kutumia mifanokutoka lugha ya Kiingereza na Kikuyu. Hata hivyo, tafiti zao zinatofautiana na huu kwani sampuli zao ni wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu wanaojifunza Kiswahili na Kiingereza kama L2, ilihali utafiti huu utachunguza athari ya lugha ya Kibosho (L1) katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili (L2).

Naye Mangwa (2005), alishughulikia athari za Kikisii kama lugha ya L1 katika uamiliaji wa Kiswahili kama L2. Aligundua kuwa kulikuwa na makosa yaliyodhihirika katika matumizi ya Kiswahili ambayo yalikuwa na chanzo chake katika lugha ya kwanza (Kikisii). Makosa yaliyobainika ni ya tahajia, sarufi na msamiati. Makosa yaliyobainika yalichangia kuwako kwa matokeo mabaya katika mtihani wa kitaifa Wilayani Kisii Kusini.

Utafiti mwingine unaokaribiana na huu wa Mangwa ni wa Obara (2014) aliyechanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wanaozungumza lugha ya Ekegusii. Utafiti wake ulidhihirisha kuwepo kwa athari za L1 kwa matumizi ya Kiswahili kama L2. Mathalani, lugha ya Ekugesii haina fonimu /l/ na, hivyo, mwanafunzi anapoandika neno kama “*lala*” hutumia fonimu inayopatikana katika lugha yake ya kwanza.

Hivyo, anaandika “*rara*’ badala ya “*lala*”. Obara alitumia Nadharia ya uchanganuzi makosa japo hakuhusisha ile ya Uchanganuzi Linganuzi kama mwenzake.

Sampuli ya Obara ilitolewa katika viwango tofauti vya kielimu, yaani wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tatu ambapo utafiti wake ulionyesha kuwepo kwa makosa katika viwango vyote. Hata hivyo, alidai kuwamakosa yalipungua kadiri mwanafunzi anavyoendelea na masomo katika viwango vya juu. Utafiti wa Mangwa na Obara, utafaa utafiti huu hasa kwa kuwa utafiti wetu unashughulikia kipengele cha kifonolojia pia. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kwa sababu utafiti wetu utajikita kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Wei (2008) alichunguza athari za usukuku katika lugha darajia kwa wazungumzaji wa lugha ya Kichina waliojifunza Kiingereza ikiwa lugha ya kigeni. Katika utafiti wake alizigawa dosari za Usukuku katika makundi matano ambayo ni dosari za usukuku katika fonolojia, sintaksia, morfolojia, semantiki na pragmatiki. Matokeo ya utafiti wa Wei yanaonyesha kwamba Usukuku ni matokeo ya mfumo tofauti wa L2 katika viwango vyote vya kiisimu tangu matamshi hadi kilongo. Aidha, alibainisha kwamba usukuku unatofautiana kati ya mjifunzaji na mjifunzaji au kati ya ujifunzaji wa lugha moja na nyingine. Hii ina maana kwamba hakuna kiwango sawa cha ufanyikaji wa dosari za usukuku. Kwa hivyo, kwa mujibu wa Wei sababu kubwa ya dosari za Usukuku kwa wajifunzaji wa lugha ya kiingereza katika jamii ya Wachina ni tofauti uliopo kati ya L1 (Kichina) na L2 (Kiingereza).

Mramba (2015) alifanya utafiti wa athari za Kirombo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika vipengele vya kifonolojia na kimofolojia ambapo athari hizo

zimesababisha ufanyaji wa dosari kwa wanafunzi wanapokuwa kwenye mchakato wa ujifunzaji lugha. Matokeo ya utafiti wake yameonyesha kuwa zipo sauti za Kiswahili ambazo katika Kirombo hazitumiki. Hivyo, kusababisha sauti hizo kutamkwa kwa sauti mbadala zilizopo katika lugha ya Kirombo. Kwa mfano, sauti /z/ ya lugha ya Kiswahili inatamkwa /s/ ambapo sauti /s/ ndiyo inayotumiwa katika lugha ya Kirombo na kusababisha neno “*mbuzi*” kutamkwa “*mbusi*” na neno “*zamani*” kutamkwa “*samani*”.

Dosari za kimofolojia zimebainika miongoni mwa wajifunzaji hao kwa mfano, upachikaji wa viambishi {-e} mwishoni mwa maneno ya Kiswahili ambapo katika Kirombo kiambishi hicho hutumika kuonesha jambo linavyotendeka kwa bidii. Aidha, utafiti wa Mramba umebaini kwamba, sababu kubwa ya dosari hizo ni mwingiliano wa L1 na L2 ambao umesababisha uhawilishaji wa sauti kutoka L1 kwenda L2. Utafiti huu umesaidia mtafiti kubaini athari za Kirombo katika ujifunzaji wa Kiswahili. Hata hivyo, kwa kuwa lugha zinatofautiana ipo haja ya kucunguza athari za Kibosho katika Kiswahili ili kubaini athari zinazojitokeza.

Wenceslaus (2015) alichunguza athari za lugha ya Kijita katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Mtafiti huyu alibaini kuwa Wajita wengi waliojifunza na wanaojifunza lugha ya Kiswahili, hukumbwa na athari za Kijita katika matumizi ya Kiswahili. Athari hizo hujitokeza katika nyanja za matamshi na maumbo, mathalani uchanganyaji wa sauti wakati wa kuzungumza na kuongeza viambishi vya maneno pasipostahili. Hivyo, baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kijita hupachika sauti /h/ au hudondosha katika baadhi ya maneno kisha kupata miundo isiyo sahihi. Mfano wa neno “*ana*” badala ya “*hana*” na “*ajaenda*”

badala ya “hajaenda”. Katika utafiti huo imegundulika kuwa sababu ya athari hizi ni kwamba katika lugha ya Kijita hakuna fonimu /h/ jambo ambalo linasababisha watu wengi kutamka maneno yenye sauti hii kwa kudondosha au kupachika pasipostabili. Athari nyingine ni uongezaji wa viambishi visivyohitajika, kwa mfano neno “*nipe-ko*” badala ya “*nipe*” na “*nimepata-po*” badala ya “*nimepata*”. Utafiti huo ulibainisha kwamba sababu kubwa ya athari hizo ni athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Utafiti huu umemsaidia mtafiti kuelewa sababu zinazosababisha L1 kuathiri L2 hasa wakati wa ujifunzaji.

Athumani (2015) alifanya utafiti kuhusu athari za kiisimu za lugha ya Kiyao katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na ukweli kwamba lugha ya Kiswahili na Kiyao zinatumiwa pamoja kwa muda mrefu hususani, maeneo ya wilaya za Songea, Tunduru na Namtumbo katika mkoa wa Ruvuma na wilaya ya Masasi katika mkoa wa Mtwara, ni dhahiri kuwa kuna maathiriano katika lugha hizi. Kwa mfano, nomino za Kiswahili ambazo zimeanza na sauti /m/ zinabadilika na kuwa sauti /n/. Wayao wanapotumia Kiswahili neno “*mjomba*” linakuwa “*njomba*” neno “*mtoto*” linakuwa “*ntoto*”. Kwa hivyo, maneno hayo yanadhihirisha kuwa lugha ya Kiyao imeathiri lugha ya Kiswahili. Vilevile, kuna maneno amabayo baadhi ya sauti zinadondoshwa na kuziacha na vokali zikiwa zinafuatana. Mathalani, neno “*baasha*” badala ya kuwa “*bahasha*” na neno “*maafali*” badala ya “*mahafali*”. Katika maneno haya, sauti /h/ hudondoshwa.

Kwa ujumla, mawazo ya wataalamu hawa yalibainisha kuwa katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya pili kuna dosari zilizojitokeza. Dosari huchangiwa kwa kiasi kikubwa na maarifa ya L1 aliyonayo mjifunzaji. Hivyo, huweza kuhamisha baadhi

ya kanuni au msamiati wa lugha ya kwanza na kuutumia katika ujifunzaji wa L2. Hali hii husababisha makosa katika ujifunzaji wa L2 kwa sababu lugha zinatofautiana. Kwa hakika, maandiko haya yalitusaidia kubaini athari za lugha mbalimbali katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hata hivyo, pamoja na kupata maarifa hayo ni ukweli usiopingika kuwa maarifa ya lugha moja hayawezi kutumika kuhitimisha lugha zingine. Hii ni kwa sababu lugha zinazotofautiana kitabia. Kwa hiyo, ipo haja ya kila lugha kuchunguzwa kimahususi. Hii ndio sababu ya utafiti huu ulikusudia kufanyika ili kutathmini athari ya lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya pili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

### **2.3 Pengo la Utafiti**

Mawazo ya wataalamu mbalimbali yanaonesha kuwa panapotokea kuathiriana kati ya lugha moja na nyingine, lugha hizo huathiriana kisarufi. Imejitokeza wazi kuwa lugha za kwanza za Kiafrika (Kibantu) huathiri lugha za pili hususani, zile za kigeni wakati wa ujifunzaji na, hivyo, kusababisha makosa ya aina mbalimbali. Aidha, kuna lugha za kigeni ambazo zimeathiriwa kwa mujibu wa wataalamu wengi kama vile Kiarabu kuathiri Kiingereza wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Hata hivyo, katika usomaji wa kazi tangulizi mtafiti alibaini kuwa hakuna uthibitisho wa mtafiti aliyewahi kushughulikia kuhusu athari za lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Hivyo, mtafiti aliona kuwa ni muhimu kuendeleza utafiti kuhusu athari za lugha za Kibantu katika kujifunza Kiswahili kwa kuangazia lugha nyingine ambazo bado hazijafanyiwa utafiti kama Kibosho. Hivyo, ili kuziba pengo hilo, utafiti huu ulilenga kutathmini “athari za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kutumia wanafunzi wa shule za msingi.”

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL) wa lugha. Nadharia ya uchanganuzi linganuzi iliasisiwa na Fries (1945) na kuendelezwa na Robert Lado (1957). Nadharia UL huchunguza athari ya lugha ya kwanza kwenye lugha ya pili. Aidha, nadharia hii huangazia ulinganuzi wa mfumo wa lugha mbili ili kubaini tofauti zinazojitokeza kati ya lugha hizo mbili. Pamoja na hayo, nadharia hii hususani, huchukulia kuwa makosa katika lugha ya pili husababishwa na athari ya lugha ya kwanza. Vilevile, wana nadharia hii wanasema kuwa nadharia hii ina uwezo wa kutambua chanzo cha kosa na kutabiri kutokea kwa makosa katika lugha ya pili (Fries, 1945).

Msingi wa nadharia hii ni kulinganisha lugha mbili zilizoingiliana katika matumizi au katika kujifunza lugha. Lengo la kulinganisha lugha hizo ni pamoja na kubainisha athari za kiisimu zinazojitokeza kwa watumiaji wa lugha hiyo husika. Nadharia hii imekubalika na baadhi ya wataalamu ambayo mawazo yao hayatofautiani na Lado (1957) bali wanaifafanua zaidi nadharia hiyo. Miongoni mwao ni James (1980) ambaye anashadadia mawazo ya Lado (1957) kwa kufafanua kuwa nadharia hii inaweza kutumika kuchanganua lugha katika vipashio mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, mofonolojia, sintaksia na semantiki. Kadhalika, anatoa wito kwa wanaisimu wengine kuwa wasiishie katika kutumia nadharia hii kuchambua vipashio vilivyobainishwa katika maelezo ya hapo awali bali wajaribu kuitumia katika kuchambua maeneo mapana zaidi kama vile matini.

Akifafanua uchanganuzi linganishi unavyopaswa kutekelezwa kwa msingi wa nadharia hii, James (1980) anabainisha kuwa ni sharti upitie katika hatua ya kutoa

ufafanuzi wa lugha zinazohusika katika darajia zinazochanganuliwa na kulinganisha ufafanuzi wa lugha zilizoathiriwa kwa ajili ya kubaini upekee wa kila lugha. Katika utafiti huu, nadharia ya UL inazingatia mambo yafuatayo. Mosi, ni kwamba athari zinazojitokeza katika lugha ya kwanza ama ya pili, husababishwa na matumizi ya lugha mbili. Pili, athari hizo zinaweza kubainishwa na kulinganisha ama kutofautisha mifumo ya lugha husika kwa kutumia UL.

Halikadhalika, ufafanuzi wa Johnson (2008) unakubaliana na Lado (1957) pamoja na James (1980). Johnson katika kufafanua nadharia hii anabainisha baadhi ya athari zinazoweza kutokea, yaani athari katika fonolojia, mofonolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki. Aidha, anafafanua kuwa licha ya msingi mkuu wa nadharia uliobainishwa na Lado (1957), kuna misingi midogomidogo ambayo ni kulinganisha athari zinazojitokeza katika lugha mbili zilizoathiriana na kutofautiana matokeo ya lugha mbili au zaidi zinazotumiwa katika jamii moja. Halikadhalika, kuyatumia matokeo ya kuathiriana kwa lugha kwa ajili ya maendeleo ya lugha hizo katika jamii husika.

Hivyo, kuwapo kwa wataalamu hao mbalimbali kumeshadadia nadharia iliyoasisiwa na Lado (1957). Kwa hiyo, nadharia hii imekuwa mwafaka katika utafiti huu kwani imetumika kubainisha makosa yanayojitokeza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Pia, mtafiti ametumia nadharia hii kwa sababu huangazia ulinganuzi wa mfumo wa lugha mbili ili kubaini athari zinazojitokeza katika lugha hizo. Hivyo, kupitia nadharia hii tumeweza kutathmini athari ya lugha ya Kibosho kama lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili hasa katika viwango vinavyochambuliwa ambavyo ni matamshi, msamiati na maana.



## **2.5 Hitimisho la Sura ya Pili**

Sura hii iligawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ilihusu mapitio ya maandiko ambapo maandiko mbalimbali yaliyohusiana na utafiti huu yamejadiliwa huku mtafiti akibainisha pengo la utafiti. Sehemu ya pili imefafanua nadharia ya uchanganuzi linganishi iliyoongoza utafiti huu. Sura inayofuata imebainisha mbinu mbalimba za utafiti zilizotumika kufikia malengo ya utafiti huu.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Vipengele vilivyofafanuliwa katika sura hii ni pamoja na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, mkabala wa utafiti, sampuli ya utafiti, usampulishaji na mbinu za kukusanya na kuchambua data.

#### **3.2 Usanifu wa Utafiti**

Usanifu wa utafiti ni mchoro, ramani na mpangilio unaoonyesha namna utafiti utakavyofanyika, tangu zoezi la kukusanya data, kuchambua data na kuandika ripoti ya utafiti (Kothari, 2004). Zipo aina mbalimbali za usanifu wa utafiti. Hata hivyo, utafiti huu utumia usanifu wa utafiti wa uchunguzi kifani. Uchunguzi kifani ni aina ya uchunguzi ambapo mtafiti huteua sehemu tu ya watafitiwa au vitafitiwa vilivyo vingi kwa lengo la kufanyia utafiti ambapo vitatoa uwakilishi wa watafitiwa au vitafitiwa vyote. Katika utafiti huu, mtafiti aliteua shule ya msingi Masoka, Kirima Juu, Boro na Kidachini. Kothari (2009) anaelezea kuwa uchunguzi kifani ni aina bora ya usanifu kwa sababu ulimfanya mtafiti kutumia muda mfupi na gharama nafuu kupata data za utafiti na kukamilisha malengo yake.

#### **3.3 Eneo la Utafiti**

Eneo la utafiti ni mahali ambapo kuna data zinazohitajika katika utafiti husika. Utafiti huu ulifanyika katika Wilaya ya Moshi Vijijini kata ya Kibosho Mashariki, vijiji vya Kirima Juu, Kirima kati, Kidachini na Boro, Mkoani Kilimanjaro. Uteuzi wa eneo hili unatokana na sababu kadhaa. Kwanza, eneo hilo ndipo lugha ya

Kibosho inapozungumzwa. Kwa hiyo, mtafiti alipata fursa ya kukusanya data katika eneo halisi la wazawa. Katika eneo hilo, mtafiti alikusanya data katika shule ambazo kutokana na utafiti wa awali ilionekana kuwa zinatimia sana lugha ya Kibosho katika mawasiliano ya kawaida wakati wawapo au wasipokuwapo shuleni. Shule nne ndizo zilizohusika katika eneo hili kama itakavyofafanuliwa katika kipengele cha sampuli na usampulishaji.

### **3.4 Sampuli ya Utafiti**

Sampuli ya utafiti ni sehemu ndogo ya kundi kubwa ambayo huteuliwa na mtafiti itumike katika utafiti wake (Kothari, 2004). Data za utafiti huu zingeweza kukusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya Moshi Vijijini lakini kutokana na ugumu wa kukusanya data kutoka shule zote za wilaya ya Moshi Vijijini, mtafiti aliteua sampuli wakilishi kutoka eneo hilo kama ifuatavyo. Kwanza, mtafiti aliteua sampuli ya shule nne kutoka Wilaya ya Moshi Vijijini. Kama tulivyoeleza awali, uteuzi wa shule hizi ulitokana na utafiti wa awali uliofanyika ili kubaini kuwapo au kutokuwapo kwa matumizi ya lugha ya asili katika shule hizo.

Pili, mtafiti aliteua sampuli ya wanafunzi na walimu waliohusika katika utafiti huu. Wanafunzi walioteuliwa walikuwa 100. Uteuzi wa wanafunzi hao ulitokana na kigezo cha kiwango cha elimu (kidarasa). Watoto 96 wanaosoma darasa la 7 ndio walioteuliwa. Hii ni kwa sababu wanafunzi hao wanauwezo wa kujibu maswali kwa njia ya mazungumzo, usaili na insha. Kila shule waliteuliwa wanafunzi ishirini na nne (24) na kufanya jumla kuu kuwa 96. Kwa upande wa walimu, mtaiti aliteua walimu 4 kutoka shule nne, yaani mwalimu mmoja kutoka kila shule.

Mtafiti amechagua makundi hayo kwa kuwa kundi la wanafunzi liliwezesha kupatikana data zilizohitajika kwa kuwa wao ndio walengwa wa utafiti huu. Kwa upande wa walimu, walioteuliwa ni wale wanaofundisha somo la Kiswahili kwa darasa la 7 kwa sababu wao wanaweza kutambua jinsi Kibosho (L1) kinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wanaofundishwa. Pia, walimu katika ufundishaji wao wanakutana na changamoto nyingi zinazotokana na wanafunzi kushindwa kufanya mawasiliano sahihi kutokana na athari ya lugha yake ya kwanza. Idadi hiyo ilitolewa kwa sababu ilitosha kutupatia data zinazohitajika katika utafiti huu. Mchanganuo wa watoataarifa ni kama unavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3.1 hapa chini.

**Jedwali 3.1: Mtawanyiko wa Sampuli ya Watafitiwa**

<u>Kundi</u>	<u>Shule</u>								<u>Jumla</u>
	<u>Masoka</u>		<u>Kirima</u>		<u>Kidachini</u>		<u>Boro</u>		
Jinsia za Watoataarifa	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	
Walimu	01	-	-	01	01	-	-	01	04
Wanafunzi	12	12	12	12	12	12	12	12	96
<b>Jumla kuu</b>									<b>100</b>

Jedwali Na. 3.1 linaonesha sampuli ya watoataarifa iliyotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Kwa hivyo, watoataarifa katika utafiti huu ni 100. Kati yao, wanafunzi ni 96 na walimu ni 4.

### **3.5 Usampulishaji**

Kothari (2004) anaeleza usampulishaji ni mchakato wa kupata sampuli au idadi ya watu au vitu vinavyoteuliwa kutoka kundi kubwa kwa ajili ya uchunguzi. Zipo aina kuu mbili za usampulishaji ambazo ni usampulishaji engwa na usampulishaji nasibu. Utafiti huu ulitumia aina zote mbili za usampulishaji ambazo ni usampulishaji lengwa na usampulishaji nasibu kama ilivyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ambapo mtafiti hulenga kutumia kundi fulani la watu ambao anaamini watampatia data anayohitaji (Kothari, 2004). Mbinu hii hutumika ikiwa kuna watu au vitu ambavyo ni muhimu kuhusishwa katika utafiti, mbinu hii ilitumika kuteua sampuli ya walimu wanaofundisha somo la Kiswahili kwa kila shule hususani, darasa la 7. Kwa hiyo, waalimu waliolengwa hapa ni wale tu waliokuwa wanafundisha somo la Kiswahili kwa darasa la 7.

Usampulishaji nasibu ni mbinu ya uteuzi wa sampuli kwa kutumia mbinu nasibu. Mbinu hizo hujumuisha aina mbalimbali za usampulishaji kama vile usampulishaji nasibu tabakishi, usampulishaji nasibu pangilifu na usampulishaji nasibu mkusanyiko. Utafiti huu ulitumia mbinu ya usampulishaji tabakisha. Kothari (2004) anafafanua kuwa usampulishaji nasibu tabakishi humsaidia mtafiti kupata sampuli ya watafitiwa anaowahitaji kwa kuwaweka katika madaraja kutegemea sifa zao na aina ya utafiti unaoshughulikiwa kisha katika kila kundi huteua idadi kadhaa ya sampuli kwa kutumia mbinu nasibu. Usampulishaji nasibu tabakishi ni mbinu ambayo humsaidia mtafiti kupata watafitiwa wale anaowataka kwa uwakilishi sawa kwa kila kundi (Kombo na Tromp, 2006). Mbinu hii ilitumika kuteua wanafunzi 96 kutoka katika shule nne. Matabaka yaliyorejelewa hapa ni ya wasichana na wavulana. Mbinu hii imetumika ili kupata wawakilishi kutoka tabaka la wasichana na wavulana. Kutoka kila tabaka, mtafiti alichagua wanafunzi 12 kwa kutumia usampulishaji nasibu.

### **3.6 Mbinu za Kukusanyia Data**

Mbinu za kukusanyia data ni mbinu mbalimbali alizotumia mtafiti kupata taarifa

zilizohusu utafiti uliofanyika. Kuna mbinu nyingi zinazoweza kutumika pamoja au kila moja peke yake kulingana na muktadha wa utafiti. Ili kufanikisha lengo kuu la utafiti huu ambalo ni kutathmini athari ya lugha ya Kibosho katika kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi, mtafiti alitumia mbinu zifuatazo katika utafiti huu.

### **3.6.1 Mbinu ya Dodoso**

Dodoso ni jumla ya maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa ajili ya kupelekwa kwa watafitiwa ili waweze kuyajibu na hatimaye kurudisha majibu (Kothari, 2004). Maswali ya dodoso yapo ya aina mbili; maswali ya maelezo na yasiyo ya maelezo. Maswali ya maelezo humtaka mtafitiwa kujieleza kadiri anavyoelewa suala aliloulizwa. Maswali yasiyo ya maelezo ni yale ambayo hayampi mtafitiwa uhuru wa kujieleza zaidi ya majibu aliyowekewa. Hivyo, mtafitiwa huchagua jibu moja kutoka katika majibu kadhaa aliyopewa kwenye dodoso. Katika utafiti huu, dodoso lilikuwa na maswali ya maelezo na yasiyo na maelezo. Maswali ya maelezo yalilenga kupata taarifa zaidi kuhusu athari za Kibosho katika Kiswahili kwa kuwaruhusu wanafunzi kuandika insha na maelezo mengine ambayo ndani yake mtafiti alichunguza athari zinazojitokeza. Uteuzi wa mbinu hii ulitokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwezo wake wa kukusanya data nyingi kutoka kwa watoataarifa wengi kwa wakati mmoja.

### **3.6.2 Usaili**

Mbinu ya usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo huwakutanisha ana kwa ana mtafiti na mtoataarifa (Kothari, 1990; Krishnaswami na Ranganatham, 2005). Hivyo, humsaidia mtafiti kupata ufafanuzi zaidi wa masuala yanayochunguzwa, hususan

yale ambayo hayawezi kupatikana kupitia mbinu nyingine kama insha na hojaji. Mtafiti alifanya mahojiano ya ana kwa ana na watoataarifa kwa ajili ya kupata data zinazohusu athari za Kibosho katika Kiswahili. Mahojiano yaliyotumika yalikuwa nusufunge (taz. Kiambatisho Na. II) kwa sababu ndiyo yaliyompa nafasi mtafiti kuuliza maswali mengi ya ziada kutokana na majibu yaliyotolewa na watoataarifa sambamba na kuomba ufafanuzi kwa baadhi ya maelezo ambayo hayakuwa wazi.

Mbinu hii ilitumika kukusanya data kutoka kwa walimu 4 pamoja na wanafunzi 96 wa darasa la 7 ambapo mtafiti aliweza kujadiliana nao masuala mbalimbali kuhusu athari za Kibosho katika kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili. Mbinu hii ilisaidia kukusanya data zilizoweza kujibu lengo mahususi la pili na la tatu. Kwa hakika, kupitia mbinu hii, mtafiti alikusanya taarifa nyingi zaidi kwa sababu watafitiwa waliweza kuuliza maswali na mtafiti alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali zaidi ikilinganishwa na mbinu nyingine kama insha na dodoso.

### **3.6.3 Mbinu ya Insha**

Insha ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambapo mtoataarifa hutakiwa kuandika maelezo au insha kuhusu jambo fulani. Katika mbinu hii ya uandishi wa insha, mtafiti aliandaa swali moja la insha ambalo watafitiwa wa darasa la saba (7) walipaswa kuandika insha isiyopungua ukurasa mmoja kuhusiana na kitu chochote ambacho hawezi kukisahau kwenye maisha yake. Watoataarifa waliachwa huru kuandika chochote. kwa sababu lengo lilikuwa dosari zaidi kuliko maudhui. Insha hizo ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mbinu hii ya insha ilitumika kwa lengo la kupata data zilimzomsaidia mtafiti katika kufikia lengo lake la kwanza ambalo kubainisha athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya

Kiswahili kwa wanafunzi wa shule ya msingi. Pia, mbinu hii ya insha ilimsaidia mtafiti kupata data zenye kuaminika na kupunguza dosari kwa kuwa mtafitiwa mwenyewe alitoa data akiwa na ung'amuzi bwete (hajui kinachoendelea) juu ya ukusanyaji wa data.

### **3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data**

Huu ni utafiti wa kitaamuli kwa sababu unahusisha zaidi maelezo pamoja na matumizi ya maarifa ya mtafiti kuhusu jambo linalotafitiwa katika uchambuzi na uchanganuzi wa data. Data katika aina hii ya utafiti huchambuliwa kwa kutumia mbinu anuwai. Mbinu mojawapo ni uchambuzi wa data kimaudhui (Kombo na Tromp, 2006). Uchambuzi wa data kimaudhui huhusisha upunguzaji wa maneno mengi yaliyokusanywa katika usaili, insha au hojaji kisha kuyapanga katika makundi yanayofanana au kuhusiana kmaudhui au kulingana na mtazamo fulani (Kombo na Tromp, 2006). Kwa hiyo, data zilizokusanywa zimewekwa katika makundi mbalimbali kwa kuzingatia maudhui yake. Data zilizohusu athari zimewekwa peke yake na zile zilizohusu mbinu za kipedagoji nazo zimewekwa katika makundi yake kisha kufafanuliwa. Aidha, upangaji wa data katika makundi pia uliongozwa na malengo mahususi ya utafiti huu. Kwa hiyo, data za kila lengo ziliwekwa peke yake na kufafanuliwa.

### **3.8 Mkabala wa Utafiti**

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo. Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni uandikaji wa taarifa kwa kutumia maelezo tu bila kuhusisha takwimu za kimahesabu. Anaendelea kusema kwamba hii haimaanishi kuwa namba hazitumiki kabisa, bali maelezo ndio yanayotiliwa mkazo. Cohen (2000) anaeleza



kuwa mkabala wa kimaelezo ni wa kupanga kutoa sababu na kuzielezea data zilizoelezewa na walengwa wa utafiti. Mkabala huu umechaguliwa kutumika katika utafiti huu kwa sababu kadhaa. Kwanza, data zilizokusanywa zimefafanuliwa kwa njia ya maelezo.

Pili, asilimia kubwa ya tafiti zinazohusu lugha kama vile isimu na fasihi na huu ukiwemo, ni za kimaelezo. Mtafiti ametumia mkabala huu kutoa kufafanua maandiko mbalimbali pamoja na ufafanuzi wa matokeo yaliyopatikana kutoka kwenye uchambuzi wa data. Kwa hiyo, mkabala wa kimaelezo umetumika kutoa maelezo ya kina kuhusu athari ya lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pamoja na kwamba mkabala wa kimaelezo umetawala lakini hii haimaanishi kuwa data au takwimu hazikuhusishwa hata kidogo. Kwa hiyo, mkabala wa kitakwimu nao kwa kiasi fulani umehusika, hususani katika utoaji wa takwimu mbalimbali pamoja na majedwali katika kufikia mahitimisho. Kwa hiyo, majedwali, takwimu na vielelezo ambavyo ni vipengele vya mkabala wa kitakwimu, vimehusika kwa kiasi fulani.

### **3.9 Itikeli ya Utafiti**

Utafiti wowote wa kitaaluma hauna budi kuzingatia masuala ya kiitikeli. Utafiti huu umezingatia masuala yote ya kiitikeli. Masuala hayo ni pamoja na uombaji wa vibali kutoka kwa mamlaka husika za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na kutoka mkoa na wilaya ambayo mtafiti alitumia kukusanya data. Baada ya kupata vibali, mtafiti aliwataarifu watoataarifa wake nia ya kufanya utafiti huu pamoja na masuala ya kimaadili yanayozingatiwa ili washiriki kutoa taarifa kwa hiyari yao wenyewe. Aidha, katika utafiti huu, taarifa zote zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti huu

zimetumika kwa masuala yanayohusu utafiti tu. Mwisho, mtafiti amechambua na kufafanua data kama zilivyokusanywa kutoka kwa watoatarifa bila kuongeza wala kupunguza. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa utafiti huu umezingatia masuala yote ya kimaadili yanayohitajika.

### **3.10 Hitimisho la Sura ya Tatu**

Sura hii imetoa maelezo kuhusu mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu, Vipengele mbalimbali kama vile usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya watafitiwa na usampulishaji vimefafanuliwa. Vipengele vingine vilivyobainiwa ni pamoja na mbinu za kukusanya na uchambuzi wa data, mkabala wa utafiti, masuala ya kiitikeli na hitimisho la sura nzima. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

## **SURA YA NNE**

### **UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA**

#### **4.1 Utangulizi**

Lengo la sura hii ni kuwasilisha na kuchambua data iliyokusanywa kuhusu athari za lugha ya Kibosho kama L1 katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa shule za msingi. Sura hii imeanza kwa kubainisha athari ya lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili kisha kufafanua sababu za wanafunzi wa Kibosho kuathiriwa wakati wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Sehemu ya tatu ya sura hii imefafanua mbinu za kipedagogia zilizobainishwa ili kupunguza athari hizo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Ufafanuzi wa masuala yote hayo umeongozwa kwa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi. Data zimechambuliwa kwa kutumia uchambuzi wa kimaudhui huku ufafanuzi ukitumika. Mwisho wa sura hii limetolewa hitimisho la sura nzima.

#### **4.2 Athari ya Lugha ya Kibosho Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili**

Lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni kubainisha athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Ili kufikia lengo hili, data zilikusanywa kutoka kwa wanafunzi kwa kutumia njia ya dodoso na insha. Watoataarifa walipewa dodoso ili wajaze pamoja na kuandika insha kuhusu jambo lolote ambalo hawezi kulisahau. Kulingana na data zilizokusanywa na kuchambuliwa, imebainika kuwa lugha ya Kibosho imeiathiri lugha ya Kiswahili katika vipengele mbalimbali vya isimu. Maoni ya watoataarifa yalionesha kuwa kuna athari mbalimbali za lugha ya Kibosho wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

Mathalani, walimu 4 waliosailiwa walieleza kuwa wanapofundisha Kiswahili kama lugha ya pili wanafunzi wao wamekuwa wakiathiriwa sana na lugha yao ya asili, yaani Kibosho. Aidha, maelezo ya dodoso pamoja na insha yameonesha kuwa kuna athari mbalimbali za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mathalani, katika insha za wanafunzi 23 kati ya wanafunzi 96, sawa na asilimia 24 zilikuwa na dosari zilizotokana na athari ya lugha yao ya kwanza, yaani Kibosho. Kwa hiyo, mjifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili huathiriwa na lugha yake ya kwanza ambayo ni Kibosho. Athari zilizobainika ni pamoja na matamshi, msamiati na maana. Ufafanuzi wa athari hizo unatolewa katika vipengele vinavyofuata.

#### **4.2.1 Athari ya Kimsamiati**

Msamiati ni jumla ya maneno yanayotumika katika lugha (TUKI, 2019). Lugha ya Kibosho na ya Kiswahili zote ni lugha za Kibantu. Hivyo, upo uwezekano wa kuingiliana kimsamiati. Hii imejidhihirisha katika utafiti huu ambapo kuna mwingiliano wa baadhi ya maneno katika lugha hizi mbili. Kwa hiyo, Wakibosho wajifunzapo Kiswahili wanapata athari chanya kwani kuna baadhi ya misamiati ambayo hutumika kwenye lugha ya Kibosho na misamiati hiyo hutumika kwenye lugha ya Kiswahili.

Hivyo, mzungumzaji wa lugha ya Kibosho anapojifunza Kiswahili inakuwa rahisi kwake. Kati ya watoataarifa, 96 ambao waliandika indha imebainika kuwa watoataarifa 35 ambao ni saw ana asilimia 37, insha zao zilikuwa na makosa ya kimsamiati yaliyotokana na athari za lugha ya kwanza ya Kibosho. Hali hii imetokana na mwingiliano wa msamiati kati ya lugha ya Kibosho na Kiswahili. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu mwingiliano wa msamiati kati ya Kibosho na Kiswahili

tutazame mifano katika Jedwali Na. 4.1

**Jedwali 4.1: Athari Chanya za Lugha ya Kibosho Wakati wa Kujifunza Kiswahili**

Na.	Kibosho	Kiswahili
1.	Kakae	Kaka
2.	Dadae	Dada
3.	Shangazie	Shangazi
4.	Mamae	Mama
5.	Babae	Baba

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Data katika Jedwali Na. 4.1 linaonesha mwingiliano wa msamiati kati ya Kibosho na Kiswahili. Baadhi ya maneno yanayotumika katika Kiswahili ndiyo hayohayo yanayotumika katika lugha ya Kibosho ingawa kuna tofauti ndogo zinazojitokeza. Tofauti hiyo ni ongezeko la kiambishi “-e” katika Kibosho ilihali kwenye Kiswahili hakuna. Mathalani, wakati Kibosho wanaita *kakae*, *dadae* au *mamae* Kiswahili wanaita *kaka*, *dada* au *mama*. Hali hii hurahisisha ujifunzaji wa lugha ya kiswahili kwa sababu msamiati waliojifunza katika lugha ya kwanza bado unatumika katika lugha ya pili. Hata hivyo, mzungumzaji hana budi kudondosha sauti *e* ili kuamka msamiati sahihi wa Kiswahili sanifu. Massamba (2007 na 2015) aliwahi kueleza kuwa upo mfanano wa lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Hivyo, athari hiyo inaonekana katika utafiti huu.

#### **4.3.1 Athari za Kimatamshi**

Habwe na Karanja (2004) na Msanjila na wenzake (2011) wanasema kuwa matamshi ni namna mtu anatumka neno au jinsi mtu anavyozungumza lugha. Muhimili wa mawasiliano mazuri ni utoaji wa matamshi yanavyoeleweka kwa msikilizaji. Katika

utafiti huu imebainika kuwa baadhi ya Wakibosho wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi wakati wanapotamka neno na badala yake kutumia matamshi yasiyo sahihi. Makosa hayo si tu hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi, bali huweza kupoteza maana ya neno lenyewe. Baadhi ya athari za matamshi zimejidhihirisha katika mbinu ya mahojiano na uandishi wa insha. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na;

#### **4.3.1.1 Athari katika Matumizi ya /s/ badala ya /z/**

Sauti /z/ ni kikwamizi cha ufizi ambacho ni ghuna. Hii ni miongoni mwa sauti ambazo hazipo katika lugha ya Kibosho. Hali hiyo ya kuathiriwa kwa /z/ sauti hiyo imesababisha wazungumzaji wa lugha ya Kibosho kutumia sauti /s/ katika nafasi ya sauti /z/ wanapojifunza Kiswahili. Sauti /s/ ni kikwamizi cha ufizi sikhuna. Wanafunzi wanaotumia lugha ya Kibosho kama L1 wameathiriwa kimatamshi wanapozungumza Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu, imegundulika kwamba wazungumzaji wa lugha ya Kibosho hutumia sauti /s/ badala ya sauti /z/ wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

Utumiaji wa sauti /s/ badala ya /z/ hujitokeza katika mazingira mbalimbali. Hii ni kutokana na watoataarifa 50 ambao ni sawa na 52% insha na madodo yao yalionesha kuwa sauti /z/ inawashinda kutumia na badala yake hutumia sauti /s/ ambao watoataarifa 46, sawa na 48% wao waliweza kutumia herufi husika kwa usahihi. Hivyo, hali hii inaonyesha kuwa katika Kiswahili kinachozungumzwa na Wakibosho, sauti /z/ inaathiriwa na sauti /s/ katika mazungumzo. Hata hivyo, sauti hizi hukaribiana kifonetiki katika kuzungumza lugha ya Kiswahili. Kwa ufafanuzi zaidi tutazame data katika Jedwali Na. 4.2.

**Jedwali 4.2: Athari Katika Matumizi ya /S/ badala ya /Z/**


Na.	Athari za Lugha ya Kibosho	Matamshi ya Kiswahili
1.	Mbusi	Mbuzi
2.	Samani	Zamani
3.	Simenishinda	Zimenishinda
4.	Chesa	Cheza
5.	Sangu	Zangu
6.	Soesi	Zoezi
7.	Wasasi	Wazazi
8.	Sisi	Zizi
9.	Saa	Zaa

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Jedwali Na. 4.2 linaonesha athari za kimatamshi ambazo zinahusisha matumizi ya sauti /s/ badala /z/ katika Kiswahili. Mithalani, wazungumzaji hutamka sauti /s/ badala ya /z/ katika Kiswahili. Kwa mfano, mzungumzaji huweza kusema sentensi *mbusi simepotea* badala ya *mbuzi zimepotea* akiwa na maana *mbuzi mnyama au mbuzi kifaa* cha kukunia nazi. Athari hii ya matamshi huweza kusababisha maana kupotea kwa sababu matumizi ya sauti /s/ badala ya /z/ husababisha neno kutokuwa na maana. Mfano mwingine ni *Samani amenitisia* badala ya kusema *Zamani alinitishia* akiwa na maana hapo muda.

Maneno mengine yaliyodhihirika katika utafiti kuwa na athari ya sauti /s/ badala ya /z/ ni *chesa* badala ya *cheza*, *sangu* badala ya *zangu*, *soesi* badala ya *zoezi*, *wasasi* badala ya *wazazi*. Neno *sisi* badala *zizi* licha ya kuathiri matamshi limeweza kuathiri hata semantiki ya maneno hayo kwani mzungumzaji alikuwa na maana ya *zizi* (sehemu ya kukaa wanyama) lakini akatamka *sisi* ambayo ina maana ya nafsi ya kwanza wingi. Vilevile, neno *saa* licha ya kuathiriwa kimatamshi pia limeathiriwa kimaana kwani mzungumzaji alikuwa na maana ya *zaa* (ongezeka kwa idadi ya watoto) lakini akatamka *saa* ambalo lina maana ya kifaa cha kuonyesha muda. Neno

*malisa* badala *maliza* neno hili limeathiriwa kimatamshi na kimaana pia maliza (kukamilisha jambo au kazi) lakini akatamka malisa ambalo linaweza kuwa na maana ya jina la mtu. Hivyo, matumizi ya sauti /s/ badala ya /z/ yanaathiri lugha ya Kiswahili kifonolojia na hata katika viwango vingine vya kiisimu kwa maana moja au nyingine. Hata hivyo, athari hizo hazijitokezi tu katika matamshi, bali pia katika uandishi kama inavyojidhihirisha katika Kielelezo Na. 4.1.



**Kielelezo 4.1: Insha Iliyoandikwa na Mwanafunzi wa Darasa la Saba**  
**Chanzo:** Data ya Uwandani (2022).

Data katika Kielelezo Na. 4.1 inaonesha namna mwanafunzi anayejifunza Kiswahili alivyoathiriwa na lugha yake ya kwanza ambayo ni Kibosho. Kama tulivyoeleza awali kuwa katika lugha ya Kibosho mzungumzaji wa Kibosho anapotumia Kiswahili hutumia sauti /s/ badala ya /z/ kwa sababu ya kuathiriwa na lugha ya kwanza. Hata hivyo, athari hii inajitokeza hata katika maandishi. Hii imejidhihirisha kupitia insha katika Kielelezo Na. 4.1 ambapo tunaona baadhi ya maneno



yameandikwa kimakosa kutokana na kuchanganya herufi /s/ badala ya /z/ katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno hayo ni *niliansa* badala ya *nilianza*, *wasasi* badala ya *wazazi*, *kasaa* badala ya *kazaa*, *nsuri* badala ya *nzuri*. Ubadilishaji nafasi wa sauti hizo licha ya kuwa na athari za kimatamshi katika lugha ya Kiswahili, huweza kusababisha athari katika vipengele vingine vya kiisimu kama vile kisemantiki kama itakavyoelezwa.

#### **4.3.1.2 Athari za Matumizi ya /s/ badala ya /dh/**

Utafiti huu umebaini kuwapo kwa athari za matumizi ya sauti /s/ badala ya sauti /dh/. Sauti /dh/ ni kikwamizi cha meno. Katika utamkaji wa sauti hii, mkondohewa hubanwa kabisa, kisha huachiwa kwa kukwamakwama wakati huo ncha ya ulimi imewekwa katikati ya meno ya juu na ya chini (Massamba, 2007). Hivyo, sauti /dh/ hutoka kwa kukwamakwama baada ya alasogezi na tuli zimegusanishwa. Katika utafiti huu, sauti /dh/ katika lugha ya Kiswahili huathiriwa na sauti /s/ ambayo ni kikwamizi cha ufizi.

Athari hii inadhihirika katika data za uwandani zilizopatikana kwa njia ya insha, usaili na dodoso. Utafiti huu umegundua kwamba katika lugha ya Kibosho fonimu /dh/ hubadilishwa na kuwa sauti /s/ kutokana na athari za lugha ya kwanza. Data kutoka ka watoataarifa inaonesha kuwa wanafunzi 60 ambao ni sawa na 62% walishindwa kutamka sauti /dh/ na badala yake walitumia sauti /s/ kutokana na athari za lugha yao ya kwanza ilihali wanafunzi 36 ambao ni sawa na 38% walitamka sauti /dh/ kwa ufasaha. Jedwali lifuatalo linawasilisha kwa muhtasari data zinazoonesha athari ya matumizi ya sauti /s/ badala ya sauti /dh/.

**Jedwali 4.3: Athari katika Matumizi ya /dh/**

Na.	Athari za lugha ya Kibosho	Kiswahili sanifu
1.	Sarau	Dharau
2.	Soruba	Dhoruba
3.	Sambi	Dhambi
4.	Saifu	Dhaifu
5.	Sulu	Dhulu
6.	Lasa	Ladha

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika Jedwali 4.3 tunaona baadhi ya maneno yanayodhihirisha utumiaji wa sauti /s/ badala ya /dh/ katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno hayo ni *sarau* badala ya *dharau*, *soruba* badala ya *dhoruba*, *sambi* badala ya *dhambi*, *saifu* badala ya *dhaifu*, *lasa* badala ya *ladha*. Ubadilishaji nafasi wa sauti hizo licha ya kuwa na athari za kimatamshi katika lugha ya Kiswahili, huweza kusababisha athari katika vipengele vingine vya kiisimu kama vile kisemantiki. Kwa mfano, neno *sulu* badala ya *dhulu* katika lugha ya Kiswahili, ambapo maana ya maneno haya ni tofauti. *Sulu* lina maana kusugua kitu kwa kusafisha ilihali *dhulu* ni kujulikana au kufahamika kwa watu wengi. Kwa hiyo, matumizi ya neno *sulu* badala ya *dhulu* katika Kiswahili ni athari kwa sababu si Kiswahili sanifu pia yanabadili maana ya neno husika. Vilevile, hali hii inadhihirisha kuwa kuathiriana kwa lugha kifonolojia huweza kusababisha ujumbe usimfikie msikilizaji kwa usahihi.

Athari hii inatokea kwa Wakibosho kwa sababu sauti /dh/ imeathiriwa na sauti /s/. Kwa hiyo, Wakiibosho wanatumia sauti /s/ ambayo ni sauti iliyokuwa karibu na hiyo kifonetiki. Ukaribu huo unatokana na kuwa sauti /dh/ ni konsonanti, inayotamkwa kwa kukwamizwa kwenye meno na huwa ni ghuna, haina unazali ilihali sauti /s/ nayo ni konsonanti inayotamkwa kwa kukwamizwa katika ufizi isipokuwa haina

ughuna. Kwa hiyo, wazungumzaji wa Kibosho wanarahisisha matumizi ya lugha kwa kutumia /s/ iliyokaribu na /dh/ kifonetiki. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu athari za Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili tutazame athari nyingine ya matamshi katika kipengele kinachofuata.

#### 4.3.1.3 Athari za Matumizi ya Sauti /f/ badala ya /v/

Utafiti huu umebaini kuwa kuna athari ya matumizi ya sauti /f/ badala ya /v/ wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Fonimu /f/ na /v/ ni vikwamizi na ni sauti za midomo meno. Vilevile, sauti hizi hutamkwa zinapokuwa zimekaribiana kiasi cha kutosha kuweza kusikika mkwaruzo unaotokea wakati hewa inapopita kati ya ala hizo. Sauti hizi hutamkwa wakati mdomo wa chini unapokuwa umeyagusa meno ya juu. Mtafiti amebaini kwamba, baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kibosho hutumia sauti /f/ badala ya /v/. Hii ni dhahiri kuwa wanafunzi wa lugha ya Kibosho wanatumia fonimu /v/ badala ya fonimu /f/. Maoni ya watoataarifa yanaonesha kuwa kati ya watoataarifa 64 sawa na 67%, walishindwa kutamka sauti /v/ na badala yake walitamka sauti /f/ ilihali watoataarifa 32 ambao ni sawa na 33%, waliweza kutamka sauti /v/ kwa usahihi katika maneno na pia katika kuandika waliandika kwa usahihi. Jedwali Na. 4.4 linaonesha athari ya matumizi ya sauti /f/ badala ya /v/ wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

#### Jedwali 4.4: Athari katika Matumizi ya Sauti /f/ badala ya /v/

Na.	Athari za Lugha ya Kibosho Matamshi yenye Athari	Matamshi Sahihi ya Kiswahili Sanifu
1.	Faa	Vaa
2.	Futa	Vuta
3.	Majifuno	Majivuno

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Jedwali 4.4 linabainisha kuwa kuna matumizi ya sauti /f/ badala ya sauti /v/ katika maneno ya kwa mfano *faa* badala ya *vaa*, *futa* badala ya *vuta*, *majifuno* badala ya *majivuno*. Kwa hiyo, sauti /f/ ikibadilishwa nafasi na sauti /v/ husababisha athari ya maana katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika neno *vaa* lenye maana ya funika mwili kwa nguo mwanafunzi anayezungumzalugha ya Kibosho anaposikika akitamka neno *faa* lenye maana ya kiwango kinachohitajika au patia mtu msaada, husababisha ujumbe usimfikie msikilizaji kwa usahihi. Athari ya sauti /f/ badala ya sauti /v/ haijitokezi katika mazungumzo tu bali imejidhihirisha pia katika maandishi. Hii imejidhihirisha kupitia insha walizoandika watoataarifa kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 4.2.

SIKU AMBOYO SIWEZI KUSATHA

Ilikuwa siku ya jumamosi tarehe 19/31/2022 dada Irine alikuja nyumbani kutoka Dar-es-salaam. Alipopika tulimwambilia sana na kujawa na puraha. Tulimpokea kwa langwe sana. Dada Irine alibutea sawadi ya ~~flatu~~ kilummoja na tulipofika tulipamdesa sana mpaka mama akabimbi a tusifae busubiri siku ya sikukuu ya krisimasi. Dada Irine alikaa wiki njima nyumbani na baadaye kunejea dar-es-salaam tulisikabika sana siku aliyokuwa anaandaka na tulimsindikisa mpaka stendi na tulipopika stendi alibupa pesa kila mmoja silingi mia tano.

**Kielelezo 4.2: Insha Iliyoandikwa na Mwanafunzi wa Darasa La Saba**

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha baadhi ya maneno yenye athari ya matumizi ya sauti /f/ badala ya sauti /v/. Kwa mfano, maneno *fiatu* badala ya *viatu*, *tusifae* badala ya *tusivae*, *tulipofaa* badala ya *tulipovaa* yanadhihirisha namna ambavyo sauti /f/ inabadilishana nafasi na sauti /v/ na kuleta maana ambayo haijakusudiwa. Sauti hizo zinapobadilishana nafasi hubadili maana na husababisha msikilizaji kushindwa kupata maana iliyokusudiwa na mzungumzaji. Mfano, neno *viatu* lenye maana ya vazi lenye lengo la kulinda na kustarehesha mguu wa binadamu wakati wa kufanya shughuli mbalimbali mzungumzaji anapotamka *fiatu* neno hilo halina maana kwenye lugha ya Kiswahili. Hivyo, msikilizaji atashindwa kupata maana iliyokusudiwa.

#### **4.3.1.4 Athari za Matumizi ya /s/ badala ya /th/**

Data za utafiti huu zimebaini pia kuna athari za matumizi ya sauti /s/ badala ya /th/. Sauti /th/ ni kikwamizi cha ulimi-meno. Sauti hii hutamkwa ikiwa ncha ya ulimi ipo katikati ya meno ya juu na ya chini. Katika utamkaji wa sauti hii, mkao wa glota huwa haubanwi kabisa bali huachiwa ili kupitisha hewa lakini kwa kugusanisha ala sogezi na ala tuli kiasi kwamba sauti kutoka kwa kukwamakwama. Sauti /s/ na /th/ zote ni vikwamizi kwa sababu hutamkwa wakati ala za sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na, hivyo, kusababisha mkwaruzo.

Maoni na data iliyokusanywa kutoka kwa watoataarifa inaonesha kuwa Wakibosho wanapojifunza Kiswahili huathiri na sauti /s/. Hii imejidhihirisha kupitiawatoataarifa 55 ambao ni sawa na 57%, kwamba sauti /th/ inawapa shida katika kutamka na kuandika. Kwa hiyo, wanapozungumza Kiswahili wanapata shida kutamka na kuandika sauti /th/ na badala yake hutamka ama kuandika /s/. Watoataarifa 41 ambao

ni sawa na 43% wao walitamka sauti /th/ inavyopaswa. Ufafanuzi zaidi wa athari hii unatolewa katika Jedwali 4.5.

**Jedwali 4.5: Athari katika Matumizi ya Sauti /S/ badala ya /th/**

Na.	Athari za Lugha ya Kibosho	Kiswahili Sanifu
1.	Selasini	The <del>l</del> athini
2.	Sawabu	Thawabu
3.	Samani	Thamani
4.	Semometa	Themometa
5.	Asiriwa	Athiriwa

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Katika Jedwali Na. 4.5 tunaona baadhi ya maneno yanayodhihirisha utumiaji wa sauti /s/ badala ya /th/ katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno hayo ni pamoja na *selasini* badala ya *thelathini*, *sawabu* badala ya *thawabu*, *samani* badala ya *thamani*, *semometa* badala ya *themometa*, *asirika* badala ya *athirika*. Ubadilishaliji nafasi wa sauti hizo licha ya kuwa na athari ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili, huweza kusababisha athari katika kipengele cha maana. Kwa mfano, neno *samani* lina maana ya vyombo vilivyoundwa kwa mbao, plastiki, miti au miyaa mfano meza, kiti, kitanda vinavyotumika nyumbani ilihali *thamani* ni ubora wa kitu kutokana na hali yake na umuhimu wake katika jamii.

Pia, matumizi ya neno *samani* badala ya *thamani* katika Kiswahili ni athari kwa sababu inabadili maana ya neno husika na inaweza kumchanganya msikilizaji ambaye hajui tatizo la mzungumzaji la kutumia sauti /s/ badala ya /th/. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu athari za kiisimu wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wanaozungumza Kibosho tutazame aina nyingine ya athari katika kipengele kinachofuata.

### 4.3.3 Athari za Kimaana

Mtafiti aliweza kubaini kuwa baadhi ya wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kibosho wajifunzao lugha ya Kiswahili mara nyingi kuna athari za maana ambazo wanazipata wakati wanapotamka baadhi ya maneno. Athari hii inahusisha upotoshaji wa maana kutokana na mabadiliko ya sauti fulani katika neno. Ingawa katika baadhi ya maelezo kuhusu athari za matamshi tumekuwa tukibainisha pia athari za maana zinazojitokeza, hata hivyo katika kipengele hiki tumetoa mifano michache ili kufafanua zaidi athari za kimaana katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Ufafanuzi uliokuwa umetolewa katika vipengele vilivyotangulia ulitokana na ukweli kwamba ni vigumu kutenganisha vipengele vya isimu kama fonolojia, mofolojia au sintaksia na kipengele cha maana. Hii ndio sababu katika baadhi ya maelezo ya makossa ya kimatamshi, maana pia imehusishwa ili kuona athari inayojitokeza. Hata hivyo, baadhi ya mifano inayohusu athari za maana kimahususi inatolewa katika Jedwali 4.6.

**Jedwali 4.6: Athari za Kimaana wakati wa Utamkaji wa Maneno**

Na.	Athari ya Kibosho	Kiswahili sanifu
1.	Kasi	Kazi
2.	Hisi	Hizi
3.	Fua	Vua

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Jedwali 4.6 linaonesha data zinazohusu athari za kimaana zinazojitokeza wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Mathalani, katika lugha ya Kiswahili neno “kazi” lina maana ya shughuli anayoifanya mtu kama kulima, kuandika, kufundisha na nyinginezo. Hivyo, mzungumzaji wa lugha ya Kibosho anapozungumza Kiswahili anaweza kutamka neno hilo “kazi” kuwa “kasi” lenye

maana ya mbio sana, upesi sana, kwa haraka mno. Hii inatokana na wazungumzaji wa Kibosho kuathiriwa na lugha ya kwanza na, hivyo, kushindwa kutamka herufi /z/. Matokeo yake ni kuwa neno hilo limeleta maana tofauti kabisa na iliyokuwa inakusudiwa hapo awali. Mfano mwingine ni neno “hizi”. Neno hili lina maana ya kivumishi kionyeshi cha ngeli (i/zi, u/zi) wingi kinachodokeza kuwa vitu vinavyotajwa vipo karibu na mzungumzaji.

Mjifunzaji wa lugha ya Kibosho kutokana na athari ya maarifa ya awali aliyonayo hujikuta anatamka “hisi” ambapo neno hili lina maana ya tambua kwa kusikia, kuona, kunusa, kuonja na kugusa. Maana hiini tofauti na maana iliyokusudiwa. Hivyo, husababisha upotoshaji wa maana iliyokusudiwa. Athari hii hutokea kwa sababu lugha ya Kibosho haina herufi /z/ badala yake hutumia /s/. Mfano mwingine ni neno “vua” lenye maana ondoa mwilini kitu kilichovaliwa, toa samaki baharini, epusha kitu au jambo, toa katika matatizo, okoa lakini mzungumzaji wa Kibosho anapojifunza lugha ya Kiswahili hutamka “fua” lenye maana ya safisha nguo kwa maji na sabuni ukitumia mikono au mashine, sinia ya ubao au chano ambayo “fua” huleta maana tofauti na iliyokusudiwa hapo awali. Baada ya kuona athari za kimatamshi na kisemantiki sehemu inayofuata inafafanua sababu za athari za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

#### **4.4 Sababu za Athari ya Lugha ya Kibosho katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili**

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilihusu sababu za athari za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Katika lengo hili, watoatarifa walitakiwa kubainisha chanzo cha sababu za athari hizo. Watoatarifa waliosailiwa walidai kuwa



kuna sababu mbalimbali zinazochangia kuwe na athari katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa mwanafunzi ambaye lugha yake ya kwanza ni Kibosho. Sababu zilizotolewa na watoataarifa walimu na wanafunzi ni uzoefu wa kutumia lugha mama na mfanano wa sarufi matamshi ya lugha hizo.

#### 4.4.1 Uzoefu wa Kutumia Lugha Mama

Utafiti huu umebaini kuwa sababu mojawapo ya kuwapo kwa athari za Kibosho katika kujifunza Kiswahili ni maarifa waliyonayo kuhusu lugha mama yao. Haya yalijidhihirisha kupitia data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya dodoso. Mtafiti alikusanya mawazo mbalimbali kutoka kwa watafitiwa ambao ni wanafunzi wa shule hizo kuhusu sababu zilizosababisha kuathiriwa na lugha ya Kibosho katika kujifunza Kiswahili. Wanafunzi 50 ambao ni sawa na 52% ya watoataarifa waliojaza dodoso, walisema kuwa lugha mama inaleta athari katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa kuwa lugha ya Kibosho inatumiwa katika mawasiliano mara kwa mara wawapo nyumbani. Hata hivyo watafitiwa 46 ambao ni sawa na 48% walisema kuwa wanafunzi wanapokuwa darasani hujifunza lugha ya Kiswahili ili kuweza kuwasiliana na watanzania na siyo kuwasiliana na kabila la Kibosho pekee. Mtafiti aliweza kubaini kuwa baadhi ya wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kibosho wajifunzao lugha ya Kiswahili, kuna athari za lugha mama zinazojitokeza katika matamshi kama sehemu ya data inavyowasilishwa katika 4.7.

**Jedwali 4.7: Athari za Kimatamshi**

<b>Na.</b>	<b>Athari za Lugha ya Kibosho</b>	<b>Kiswahili Sanifu</b>
1.	Samani	Thamani
2.	Sawabu	Thawabu
3.	Sote	Zote
4.	Majifuno	Majivuno

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Jedwali 4.7 linaonesha baadhi ya maneno yenye athari ya matamshi yanayotokana na mzungumzaji kuathiriwa na lugha mama yake. Sababu kuu ya athari za kimatamshi ni ndimi za wahusika kuathiriwa na lugha mama pamoja na kukosekana kwa sauti /z/, /th/, /dh/ na /v/ katika lugha ya Kibosho. Matokeo haya ya utafiti yanathibitisha alichosema Matinde (2012) kuwa kila mtu hujifunza na kumudu mfumo wa lugha yake ya kwanza lakini anapoanza kujifunza lugha nyingine hutumia mfumo wake wa lugha ya kwanza aliouzoa kuweza kujifunza lugha ya pili. Kwa kufanya hivyo, ni lazima lugha ya pili (Kiswahili) iathirike kwa sababu maandishi, mpangilio wa vipashio pamoja na sauti ya lugha hiyo ya pili zilitamka na kuandikwa isivyo sahihi.

Naye Cruse (1985) aliwahi kudai kuwa makosa mengi katika lugha ya pili huwa na ufananisho wa lugha ya kwanza. Anaendelea kusema kuwa makosa hayo ni kutokana na watu wanapojifunza lugha ya pili huwa tayari wanayo lugha ya kwanza. Hivyo, hutumia kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza wakati wa mazungumzo na uandishi wa lugha ya pili. Kutokana na hali hii ya kuwa na mazoea ya kutumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili imekuwa ni chanzo cha kuathiri lugha ya pili katika usemaji na uandishi. Changamoto hii ndio inayowapata watumiaji wa lugha ya Kibosho wanapozungumza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Sababu hii iliwahi pia kubainishwa na Otiende (2013) kuwa lugha mama huathiri lugha ya Kiswahili. Sovu (2011) aliwahi kueleza kuwa lugha ya Kiswahili iliathiriwa na lugha Kiha katika matamshi na hata maandishi.

#### **4.4.2 Athari za Sarufi Matamshi katika Lugha ya Kibosho**

Sarufi matamshi hushughulika na mfumo wa sauti katika lugha fulani. Hyman (1975) anaelezea kuwa tawi hili lina maana kama mtaala wa mfumo wa sauti, yaani

linashughulikia jinsi sauti zinavyopangwa pamoja na uamilifu wake katika lugha mahususi. Kwa hiyo, athari zilizoshughulikiwa katika kipengele hiki ni zile zinazoathiri matamshi au sauti (fonimu) za lugha mahususi kama ilivyo kwa lugha ya Kibosho katika lugha ya Kiswahili sanifu. Kwa mfano, watumiaji wa lugha ya Kibosho walibadilisha sauti za lugha ya Kiswahili wakati wa utamkaji na kusababisha athari kubwa katika lugha kwani sauti hizi zinapotamkwa isivyo sahihi hubadilisha na kupotosha maana halisi ya neno.

Katika kipengele hiki, jumla ya watafitiwa 96 walihojia. Kati ya hao watafitiwa 70 ambao ni sawa na 73% walikubaliana na hoja hii kwa maelezo ya kwamba kuna baadhi ya sauti za Kibosho zinakosekana kwenye lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 26 ambao ni sawa na 27% hawakukubaliana na hoja hiyo. Asilimia 73% ya watafitiwa waliyokubaliana na sababu hii walipohojiwa na mtafiti kwa nini walikubaliana hivyo walisema kuwa, sauti wanazoshindwa kuzitamka pamoja na kuandika kwa usahihi ni zile ambazo hazipatikani kwenye lugha yao ya kwanza ambazo ndizo zinazotakiwa kutamka katika maneno ya Kiswahili.

Baadhi ya sauti ambazo zilionekana kuwa ni changamoto kwao kuzitamka ni pamoja na /th/, /z/, /dh/ pamoja /v/. Sababu ya kushindwa kutamka sauti hizi za lugha ya Kiswahili ni kutokana na lugha ya Kibosho kutokuwa na sauti hizoMfano walisema:

- i. Badala ya kutamka /za/ wanasema /sa/
- ii. Badala ya kutamka /tha/ wanasema /sa/
- iii. Badala ya kutamka /dha/ wanasema /sa/
- iv. Badala ya kutamka /va/ wanasema /fa/

Matokeo haya ya utafiti wetu ambao watafitiwa walikubaliana na sababu ya kukosekana kwa baadhi ya sauti katika lugha ya Kibosho, mawazo hayo yanakubaliana kabisa na tafiti zilizotangulia. Mathalani, Wenceslaus (2015) aliwahi kueleza kuwa lugha ya Kiswahili imeathiriwa na lugha ya Kijita. Kuathiriwa huko kunatokana na kutumia lugha ya Kijita kwa asilimia kubwa kuliko kutumia Kiswahili. Pia, Sovu (2011) aliwahi kubainisha kuwa watumiaji wa lugha ya Kiha walikosea kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha kutokana na ukosefu wa baadhi ya sauti katika lugha yao Kiha na kusababisha kuiathiri lugha ya Kiswahili wakati wanapozungumza.

#### **4.5 Mbinu za Kipedagogia Katika Kusahihisha Athari za Wanafunzi**

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu lilikuwa kuainisha mbinu za kipedagogia katika kusahihisha athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili. Ili kufikia lengo hili, data zilikusanywa kutoka kwa watoatarifa ambao ni walimu wanaofundisha Kiswahili darasa la 7. Kama ambavyo tumejadili katika kipengele cha 4.3 kuwa lugha ya kwanza ndio chanzo kikubwa cha athari za mjifunzaji wa lugha ya pili. Wajifunzaji wa lugha ya pili wanapojifunza lugha hiyo huathiriwa na sarufi ya lugha chanzi. Hivyo, kufanya makosa wakati wanajifunza. Imeelezwa kuwa matumizi ya lugha ya Kibosho husababisha wanafunzi kuathiriwa wakati wa kujifunza Kiswahili kama L2. Utafiti huu unapendekeza mbinu zifuatazo za kipedagogia katika kusahihisha athari za wanafunzi wazungumzaji wa Kibosho kama L1 kwa wanaojifunzaji lugha ya Kiswahili kama L2.

##### **4.5.1 Walimu Wawaelekeze Wanafunzi Utamkaji Mzuri wa Matamshi**

Kazi mojawapo ya mwalimu ni kuhakikisha wanafunzi wanaelewa lugha kwa

ufasaha. Walimu wanapaswa kuwaelekeza wanafunzi nini cha kufanya na nini asifanye. Kwa hiyo, ipo haja ya walimu kuwasaidia wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi ili waondokane na hali ya kutamka maneno ya Kiswahili kwa makosa. Haya yalibainishwa na maoni ya watoataarifa 04 ambao ni walimu kuwa kila mwalimu anapaswa kuwasaidia wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi kwa kuzingatia misingi ya lugha ya Kiswahili. Waliongeza kuwa wanafunzi wanapaswa kurekebisha pindi wanapokosea kwenye utamkaji wa maneno kwa kuwasaidia kutamka kwa usahihi.

Wanafunzi wapewe mazoezi ya mara kwa mara kuhusu utamkaji sahihi wa maneno hayo na waelezwe sababu za dosari hiyo ambayo ni kuwapo kwa tofauti za sauti kati ya Kiswahili na Kibosho. Hivyo, kwa kuwa lugha wanayopaswa kuitumia ni Kiswahili, hawana budi kufuata utaratibu huo wa matamshi. Kwa kufanya hivi hapana shaka wanafunzi wenye athari za matamshi watakuwa na welewa na matamshi sahihi kulingana na utaratibu za sarufi ya Kiswahili sanifu. Kwa ujumla, mtafiti anapendekeza kuwa wanafunzi wafundishwe vizuri wanapokuwa darasani juu ya matamshi sahihi ya maneno ya Kiswahili ili kuondoa tatizo la athari katika lugha ya kwanza.

#### **4.5.2 Utoaji wa Elimu kuhusu Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili**

Pendekezo lingine ni elimu itolewe kwa wanajamii kuhusu umuhimu wa kuzungumza Kiswahili fasaha. Hapana shaka wanajamii wengi hawafahamu umuhimu wa kuzungumza Kiswahili fasaha na kuwa rekebisha wale wasioweza kuzungumza vizuri. Hivyo, ikiwa elimu itatolewa hapa shaka kuwa itasaidia

wanajamii kufahamu lugha hiyo na kuwasaidia wale wasio na matamshi sahihi. Elimu hiyo inaweza kutolewa kwa kuandaa makongamano na warsha. Pendekezo hili lilitolewa na watafiti walimu wakati wa majadiliano na mtafiti.

Watoataarifa hao walidai kwamba jamii nyingi ikiwemo ya Kibosho hazijui umuhimu wa kuzungumza lugha ya Kiswahili hasa wawapo nje ya mazingira ya shule. Kama wangekuwa wanajua umuhimu wa kuzungumza lugha ya Kiswahili tuna hakika kuwa wangeiheshimu, wangeipenda, kuidumisha na kuendeleza katika matumizi. Watoatarifa hao waliendelea kufafanua na kueleza kwamba, hali ya kutoithamini lugha ya Kiswahili hasa wanapokuwa mazingira ya nje na shule inachangia lugha hii kuonekana kutokuwa na umuhimu.

Wazungumzaji wa Kibosho wanapaswa waelimishe juu ya umuhimu wa lugha ya Kiswahili hasa inavyotumika kwa sasa kimataifa. Pia, wapewe na kufanya mazoezi ya kutosha ya kukisoma na kukiongea Kiswahili kwa ufasaha. Hoja hii ya kutolewa mafunzo mbalimbali pia ilitolewa na baadhi ya wanafunzi waliohojiwa. Wanafunzi hawa walidai kuwa wao hawaoni umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu wawapo nje ya mazingira ya shuleni wazazi wao huwasiliana nao kwa kutumia lugha ya Kibosho. Hivyo basi, kama mafunzo mbalimbali yatatolewa kwa wanafunzi wa Kibosho juu ya kukipenda na kuzungumza lugha ya Kiswahili wawapo shuleni na nje ya mazingira ya shule, itasaidia sana kupunguza athari ya lugha ya Kibosho katika kuzungumza lugha ya Kiswahili. Pia, katika warsha na makongamano zitolewe motisha pamoja na tuzo mbalimbali kwa zile shule zenye wanafunzi wanaozungumza Kiswahili kwa ufasaha.

### **4.5.3 Watoto Wafundishwe Lugha ya Kiswahili Tangia Utotoni**

Mjuzi bora wa lugha huanzia utotoni. Kwa hiyo, lugha inapaswa kufundishwa tangu utotoni. Maelezo haya yana maana kuwa unapoanza kumfundisha mtoto matumizi bora ya lugha tangu akiwa mtoto ndivyo unavyomuimarisha kimatumizi. Kwa hiyo, wazazi na walezi hawana budi kuwafundisha watoto wao lugha ya Kiswahili hususani wakati wanazaliwa. Haya yamebainishwa na watoataarifa 80 sawa 83%, kuwa suala la kujifunza Kiswahili linapaswa kufundishwa tangu utotoni ili kumjengea mwanafunzi uwezo mzuri wa kufanya mawasiliano. Waliendelea kudai kuwa wazazi au walezi wa watoto hao wahamasishwe ili waweze kutumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana nao na waondoe fikra potofu kuwa mtoto kujua Kiswahili ndio chanzo cha kupoteza utamaduni wa kabila lao au jamia yao.

Kwa hiyo, iwapo wazazi au walezi, watahamasishwa kwa pamoja, ni wazi kuwa watoto wao watakuwa wazungumzaji wazuri wa lugha ya Kiswahili. Asilimia kubwa ya wanafunzi walitaja sababu hiyo kuwa itapunguza athari ya lugha Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, wazazi au walezi wahamasishwe ili waweze kutumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana na watoto wao pamoja na kuondoa imani potofu kuwa mtoto anapojifunza lugha ya Kiswahili ndiyo chanzo cha kupoteza utamaduni wao. Ikiwa jitihadi zitafanyika ni dhahiri kuwa watoto watakuwa wazungumzaji wazuri wa lugha ya Kiswahili.

## **4.6 Hitimisho la Sura ya Nne**

Sura hii ilihusika na uwasilishaji, ufafanuzi na uchanganuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Uwasilishaji na uchanganuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Matokeo yameonyesha kuwa lugha ya Kibosho

imeathiri sana lugha ya Kiswahili kimsamiati, kimatamshi na kimaana. Aidha, tumejadili sababu zilizochangia lugha ya Kibosho kuathiri Kiswahili pamoja na kubainisha mbinu za kipedagogia zinazoweza kutatua athari hizo. Utafiti huu unadhihirisha kuwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kibosho hukumbana na changamoto mbalimbali wakati wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili.



## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA TUTAFITI**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni utangulizi, muhtasari wa utafiti, hitimisho la utafiti pamoja na kubainisha mapendekezo mbalimbali ya utafiti. Ufafanuzi wa vipengele hivyo unatolewa katika vipengele vinavyofuata.

#### **5.2 Muhtasari wa Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza athari za lugha ya Kibosho katika kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu. Lengo la kwanza lilikuwa ni kubaini athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Lengo la pili lilikuwa ni kutathmini sababu za athari za kiisimu za lugha ya Kibosho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na lengo la tatu lilihusu kuanisha mbinu za kipedagogia katika kusahihisha athari za Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Utafiti huu ulifanyika katika Wilaya ya Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro na ulihusisha watoataarifa 100 ambao ni wanafunzi 96 na walimu 4 kutoka shule za Masako, Boro, Kidachini na Kirima Juu.

Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za dodoso, usaili na mbinu ya insha. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui huku tukiongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Kulingana na uchambuzi wa data, matokeo ya utafiti huu yanafafanuliwa kama ifuatavyo. Kwanza, katika lengo mahususi la kwanza ambalo lilihusu kubainisha athari za Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili, athari mbalimbali zilibainika. Athari hizo

ni pamoja na athari za kimsamiati, kimatamshi na kimaana. Kwa upande wa msamiati imebainika kuwa baadhi ya misamiati inayotumika kwenye lugha ya Kibosho hutumika vivyo hivyo kwenye lugha ya Kiswahili hivyo wakibosho wajifunzao Kiswahili hupata urahisi.

Kwa upande wa matamshi imebainika kuwa baadhi ya wakibosho wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi ya sauti wakati wanapotamka neno badala yake hutumia matamshi yasiyo sahihi. Makosa hayo si tu hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi, bali pia huweza kupoteza maana ya neno lenyewe. Baadhi ya wanafunzi wa Kibosho hutumia sauti /s/ badala ya sauti /z/ sauti /s/ badala ya sauti /dh/, sauti /f/ badala ya sauti /v/. Athari hii inatokana na hali ya kukosekana kwa baadhi ya sauti katika lugha ya Kibosho na Kiswahili.

Kwa upande wa maana imebainika kuwa makosa ya kimatamshi pia husababisha makosa ya kimaana. Hii ni kwa sababu wazungumzaji wanapobadili sauti moja husababisha maana nzima kubadilika. Wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kibosho wajifunzapo lugha ya Kiswahili kuna baadhi ya sauti ambazo husikika kwenye maneno ambazo sauti hizo hubadili maana asilia ya neno. Mathalani, mzungumzaji anapotamka neno “hisi” badala ya “hizi” huleta maana tofauti kutokana na lugha ya Kibosho kutokuwa na sauti /z/ na badala yake hutumia sauti /s/.

Kwa upande wa lengo mahususi la pili ambalo lilikuwa ni kuabinisha sababu za zinazosababisha athari hizo. Sababu zilizobainika ni pamoja na wazungumzaji wanafunzi kuwa na uzoefu wa kutumia lugha mama na athari za sarufi matamshi katika lugha ya Kibosho ambapo kuna ukosekanaji wa sauti /z/, /dh/ na /v/ katika

lugha hiyo.

Kwa upande wa lengo la tatu ambalo lilikuwa ni kubainisha mbinu za kipedagiko za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wakibosho wanaojifunza Kiawahili kama L2. mbinu zilizobainishwa ni pamoja na walimu wawaelekeze wanafunzi utamkaji mzuri wa matamshi, yaandaliwe makongamano, warsha na mafunzo mbalimbali kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili na watoto wafundishwe lugha ya Kiswahili tangia utotoni.

### **5.2.1 Mchango wa Utafiti**

Utafiti wa kitaaluma hufanyika kwa lengo la kuongeza maarifa katika uwanja husika, miongoni mwa madhumuni mengine. Huu ni utafiti wa kitaaluma ambao umechunguza athari za Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Hivyo, una mchango kitaaluma, hususan katika uwanja wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwanza, utafiti huu umebainisha athari za Kibosho katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Maarifa haya kuhusu athari za Kibosho katika kujifunza Kiswahili yatawasaidia walimu pamoja na wanafunzi kufahamu namna lugha ya Kibosho inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kamalugha ya pili.

Pili, utafiti huu umebainisha mbinu za kipedagoji zitakazo saidia kuondoa athari hizo. Kwa hiyo, maarifa ya namna ya kuondoa athari za lugha ya asili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili yatawasaidia wahusika kama walimu na wanajamii kufahamu namna ya kukabiliana na athari hizo. Kwa hiyo, kukamilika kwa utafiti huu kumechaangia maarifa kuhusu lugha ya Kibosho inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Ni dhahiri kuwa maarifa haya yatasaidia kuboresha elimu hasa kwa kuwa wahusika wataweza kufahamu namna ya kuondoa makos ana

kuzungumza Kiswahili fasaha.

### **5.3 Hitimisho la Utafiti**

Utafiti huu unahitimisha kwamba kuna athari za kimsamiati, kimatamshi na kimaana zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya L2 katika jamii ya Wakibosho. Athari hizo zinasababisha matumizi yasiyo sanifu ya lugha ya Kiswahili. Pamoja na hayo, utafiti huu umebaini sababu mbalimbali za athari hizo. Sababu hizo ni pamoja na uzoefu wa kutumia lugha mama pamoja na athari za sarufi matamshi katika lugha ya Kibosho. Mwisho, utafiti huu umependekeza mbinu mbalimbali za kuondoa au kupunguza athari hizo. Mbinu hizo ni pamoja na walimu kuwaelekeza wanafunzi utamkaji mzuri wa matamshi, utoaji wa elimu kuhusu umuhimu wa Kiswahili kupitia makongamano, warsha na mafunzo mbalimbali kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili na watoto wafundishwe lugha ya Kiswahili tangia utotoni.

### **5.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Utafiti huu unatoa mapendekezo ya jumla na ya tafiti fuatishi. Ufafanuzi wa mapendekezo hayo unatolewa katika vipengele vinavyofuata.

#### **5.4.1 Mapendekezo ya Jumla**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mtafiti anapendekeza kutolewa elimu ya juu ya umuhimu wa kuzungumza lugha ya Kiswahili katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Hii ni kutokana na watu mbalimbali hasa wakazi wa maeneo ya vijijini ambao baadhi wamekuwa wakidharau lugha ya Kiswahili na kuona haina thamani kwao. Mtafiti anapendekeza pia kuwepo kwa mashindano ya ndani baina ya darasa moja na jingine ya uandishi wa insha kwa kutumia lugha ya Kiswahili kisha

kubainisha makosa yanayojitokeza katika insha hizo. Hii itasaidia kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili shuleni. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuzuia Kiswahili kisiendeleo kuathiriwa na lugha za asili. Pia, shule zitengeneze kanuni ndogondogo za kuweza kuzitumia kama njia ya kuweza kuwasaidia watoto kuongea Kiswahili kama kubandika mabango yanayohimiza kuongea Kiswahili au kuwa na kibao cha kuvalisha wale wanaoongea Kibosho kama kile kinachotumika katika lugha ya Kiingereza SPEAK ENGLISH na hiki kiandikwe ONGEA KISWAHILI. Aidha, shule zinaweza kuorodhesha maneno yenye makosa na sahihi kutokana na athari nyingi zinazojitokeza kisha kubandika kwenye mbao za matangazo kwa ajili ya wanafunzi kujisomea. Pia, klabu za masomo zinaweza kutumiwa kuhamasisha matumizi sahihi ya Kiswahili sambamba na kubainisha dosari zinazofanywa na wanajamii husika.

#### **5.4.2 Mapendekezo kwa Tafiti Fuatishi**

Mtafiti anapendeza kuwa tafiti nyingi zifanyike ili kuweza kuibua maarifa mapya kuhusiana na namna lugha za asili zinavyoweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hii itasaidia kujua ni namna gani tunaweza kuepuka na kuhifadhi Kiswahili kisiathiriwe na lugha za asili.

### MAREJELEO

- Athumani, M. R. (2015). Athari za Kiisimu za Lugha ya Kiswahili katika Lugha ya Kiyao. Tasnifu ya M.A, (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Huria Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.
- Bartoo, J. P. (2004). *Acquisition of English Syntax by Keiyo LI Speakers*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya, Nairobi, Kenya.
- Bosha, I. (1993). *Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya*. Dar es Saalam: Dar es Saalam University Press.
- Brown, H. D. (2000). *Principles of Language Learning and Teaching*. New York: Longman.
- Cohen, L. (2000). *Research methods in Education*, 5<sup>th</sup> Eedition. London: Rutledge Farmer.
- Corder, S. P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*. London: Oxford University Press.
- Cruse, D. A. (1986). *Lexical Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Enon, C. J. (1998). Education Research and Measurement. Department of Distance Education. Makerere University.
- Fries, C.C. (1945). *Teaching and Learning English as a Foreign Language*. Ann Arbor: University of Michigan Press.
- Fromkin, V. Rodman, R. na Hyams, N. (2007). *An Introduction to Language* (8th ed). Boston: M.A: Thomson Wadsworth.
- Jonker, J. and Pennink, B. (2010). *The Essence of Research Methodology: A concise Guide for Masters and Ph.D Students in Management Science*. Neither Land:

Springer

- Joy, M.S. (2012). Causes of Syntactical Errors in Kiswahili Second Language Learning among Western Kenya's Kiidakho First Language Speakers. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies (JETERAPS)* 3(6), 921-928.
- Kombo, D. K. and Tromp, D. L. (2006). *Propasal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Komunte, B. S. (2001). The Impact of Bantu Languages in English Language Learning Processes in Tanzania Secondary Schools. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili*, 2000, 287-296.
- Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd Publishers.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods of Techniques*, 2<sup>nd</sup> Ed., Indi: New Age International (P) Ltd Publishers.
- Krashen, S. D. na Tracy, D.T. (1983). *The Natural Aproach Language Acquisition in the lassroom*. Oxford: Pergamon Press.
- Lado, R. (1957). *Linguistics across Cultures*. Ann Arbor: University of Michigan Press
- Lusesa, J. (2013). *Athari ya Lugha ya Kisukumu katika ujifunzaji wa Kiswahili (Tasnifu)*; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.
- Mangwa, D. O. (2015). *Athari za Ekegusi Katika Kiswahili na Zinazochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi wa Kisii Wilayani Kisii Kusini. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Egerton.

- Massamba, D. P. B. (1977). A comparative study of Ruri, Jita and Kwaya Languages of the Eastern Shores of Lake Nyanza, (unpublished) M.A Dissertation. University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, D. P. B. (1986). On the influence of Local Languages on Kiswahili: The Case Study of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53/1 na 53/2, 67-83.
- Mbwesa, K. J. (2016). *Introduction to Management Research. A Handbook*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mpangala, G. (2018). Athari ya Lugha ya Kimakonde katika kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tasnifu (haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kitivo cha Sanaa na Sayansi na Jamii.
- Mramba, T. P. (2015). Uchunguzi wa Athari za Kirombo Katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Mukuthuria, J. K. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na wanafunzi wa Kiitigani Kenya. Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Ng'ang'a, W. (2002). Makosa ya Kisarufi Katika Insha ya Wanafunzi na jinsi yanavyoshughulikiwa na Walimu Katika Tarafa ya Ndaragwa. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Ngugi, J. K. (2007). Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wakikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.



- Nyanda, J. (2015). Athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Tasnifu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Kitivo cha sanaa na Sayansi ya jamii.
- Obara, J. M. (2014). Uchanganuzi wa Makosa Yaliyofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Nairobi.
- Onyango, J. O. (1997). Uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha Wanafunzi wa Kinyala: Mtazamo wa uchanganuzi linganuzi (Master thesis and Dissertation). Kenyatta University Institutional Repository. School of Humanities and Sciences. Department of Kiswahili and African Languages.
- Otiende, M. A. (2013). Athari za Kimofonolojia ya Kibasuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kama Lugha ya Pili (Tasnifu). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Richards, J. C. (1974). Error Analysis and Second Language Strategies. In J. H. Schumann and N. Stenson (Wah.) *New Frontiers in Second Language Learning*. Rowley: Mass Newbury House.
- Selinker, L. (1972). *Inter Language*. New York: Rawlence Erlbaum Associates.
- Sovu, A. Y. (2011). *Matumizi ya Kiha katika Kiswahili cha Mazungumzo*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Dar es Saalam, Tanzania.
- Wenceslaus, M. (2015). Athari ya *Lugha* ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili (Tasnifu). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

## VIAMBATANISHO

### **Kiambatanisho 1: Maswali kwa wanafunzi wa Kibosho wa shule za msingi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili**

Mimi ni Mwanafunzi wa somo la isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya Athari ya lugha ya Kibosho (Kiw'oso) katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya shahada ya Uzamili. Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswahili haya ili yasaidie kukamilisha utafiti huu. Natanguliza shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano wako.

Umri.....

Jinsia.....

Kiwango cha elimu.....

### **Maswali: Soma maswali na majibu yafuatayo kisha chagua herufi ya jibu sahihi na kuiandka katika kisanduku**

1. Je, wewe lugha yako ya kwanza ni kibosho (kiw'oso)?  

A. Hapana	B. Ndiyo	[     ]
-----------	----------	---------
2. Je, Kiswahili ni lugha ya pili kwako?  

A. Hapana	B. Ndiyo	[     ]
-----------	----------	---------
3. Uwapo nyumbani unapendelea kutumia lugha gani?  

A. Kibosho(kiwo'so)	B. Kiswahili	[     ]
---------------------	--------------	---------
4. lugha gani unapendelea itumike kufundishia shuleni?  

A. Kibosho	B. Kiswahili	[     ]
------------	--------------	---------

5. Kwa ujumla nini kifanyike ili kuwasaidia wanafunzi wa Kikibosho waweze kujifunza Kiswahili kwa ufasaha? Eleza kwa ufupi.

.....

.....

.....

.....

**Kiambatanisho 2: Dodoso kwa WalimuWalimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi**

Mimi ni mwanafunzi wa Kiswahili wa Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Huria Tanzania. Nafanya utafiti kuhusu Athari ya ya Lugha ya Kibosho katika kujifunzi lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi ikiwa ni sehemu ya masharti ya kukamilisha sehemu ya masomo yangu. Ukiwa kama mwalimu unayefundisha somo la Kiswahili ninaomba msaada wako ili kukamilisha utafiti huu. Ninatangulizi shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano wako.

**Dodoso kwa walimu wa Kiswahili**

Jina.....

Umri.....

Jinsia.....

Kiwango cha elimu.....

**Tafadhali chagua herufi ya jibu sahihi na pia jaza nafasi zilizo wazi;**

1. Wanafunzi unaowafundisha wanao uwezo wa kuzungumza Kiswahili fasaha?

a. Ndiyo                      B. Hapana                      [        ]

Toa sababu kwa jibu ulilochagua.

I. ....  
.....

II. ....  
.....

III. ....  
.....

2. Wakati wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili matumizi ya lugha ya Kibosho ni ya kiwango gani?

A. Kikubwa      B. Kati      C. Kidogo      D. Hakuna      [      ]

3. Je, kuna athari yeyote ya kimsamiati, kimatamshi na kimaana inayosababishwa na Kibosho katika kujifunza Kiswahili?

A. Ndiyo      B. Hapana

Iwapo jibu ni ndiyo, toa mifano mitatu kwa kila kipengele ili kudhihirisha athari hizo:

a) Athari za msamiati

Lugha ya Kibosho	lugha ya Kiswahili
------------------	--------------------

Babae	baba
-------	------

Mamae	mama
-------	------

Kakae	kaka
-------	------

Taja misamiati mingine iliyoathiri lugha ya Kiswahili.

.....

.....

b) Athari za kimatamshi

I. Kupachika fonimu /s/ badala ya /z/

Mfano mbusi badala ya mbuzi

Hisi badala ya hizi

II. Kupachika fonimu /g/ badala ya /gh/

Mfano gafla badala ya ghafla

Garama badala ya gharama

Taja athari nyingine unazozifahamu.

c) Athari za kimaana na mifano

I. ....  
.....

II. ....  
.....

III. ....  
.....

4. Ni sababu zipi huchangia kuwaathiri wanafunzi wakibosho katika kujifunza

Kiswahili kama lugha yao ya pili? Taja sababu nne;

I. Athari ya lugha mama

II. Athari katika mazingira

Taja na nyingine unazozifahamu;

.....  
.....

5. Unakumbana na changamoto zipi wakati unapowafundisha wanafunzi

wakibosho lugha ya Kiswahili? Yataje na kisha elezea kwa ufupi.

I. Utamkaji usio sahihi wa matamshi ya Kiswahili

II. Wanafunzi kutokujengewa msingi mzuri wa usomaji wa vitabu vya  
hadithi kuazia darasa la awali

Taja na nyingine unazozifahamu;

.....  
.....

6. Mbinu au hatua gani ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuwasaidia wanafunzi wakibosho kujifunza Kiswahili kwa ufasaha?

- I. Watoto wafundishwe lugha ya Kiswahili tangia utotoni
- II. Wazazi wawe vielelezo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili

Taja na nyingine unazozifahamu;

**Kiambatisho cha 3: Maswali ya usaili kwa wanafunzi**

1. Je, lugha yako ya kwanza ni lugha ya Kibosho?
2. Je, unajua kuzungumza lugha ya Kibosho (Kiw'oso) vizuri?
3. Uwapo nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?
4. Je, ni lugha ipi unapendelea itumike kufundishia masomo?
5. Unafikiri ni sababu zipi zinazosababisha uchanganye lugha ya Kibosho na lugha ya Kiswahili wakati unapozungumza?
  - i. Matumizi ya mara kwa mara ya lugha mama
  - ii. Utumiaji wa baadhi ya misamiati ya lugha ya Kibosho kwenye lugha ya Kiswahili

Taja na nyingine unazozifahamu;

.....

.....

.....



**Kambatanisho 4: Bajeti ya Utafiti**

Shughuli ya utafiti ina mahitaji mbalimbali ambayo ni muhimu ili kukamilisha mchakato wa utafiti. Ili kufanikisha shughuli hii mtafiti, ameandaa bajeti ya utafiti ili kuweza kufikia malengo ya utafiti. Ifuatayo ni bajeti ya utafiti.

<b>Na.</b>	<b>Shughuli au kifaa</b>	<b>Gharama kwa kifaa</b>	<b>Jumla</b>
1	Kuchapa pendekezo	Sh. 400 @ x 60	24, 000/=
2	Vifurushi vya mtandao	20, 000/=	20, 000/=
3	Vifaa vya ukusanyaji wa taarifa <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Shajara na karatasi</li> <li>➤ Karamu za wino ishirini</li> <li>➤ Kinyonyi kimoja</li> </ul>	5, 000/=	5, 000/=
		2 00/= @	4, 000/=
		20, 000/=	20, 000/=
5	Nauli kwa ajili ya ukusanyaji wa data	250,000/=50, 000/=	250,000/=50, 000/=
6	Chakula	30, 000/=	30, 000/=
7	Kuhariri tasnifu kurasa 100	Kila ukurasa 5000	500,000/=
8.	Kuaandaa Tasnifu kwa ajili ya utahini. Kutoa nakala na Kujalidi tasnifu	100,000	100,000/=
9.	Kuandaa tasnifu kwa ajili ya kukabidhi nakala 6 za tasnifu. Kutoa nakala na kujalidi tasnifu	350,000	350,000
	<b>Jumla</b>		1,153,000/=

## THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

### DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES

P.O.BOX 23409  
DAR ES SALAAM, Tanzania  
<http://23409www.openuniv>



Tel: 255-22-2668992/2668445  
Ext.2101  
Fax:255-22-2668759  
E-mail: [dpps@out.ac.tz](mailto:dpps@out.ac.tz)

**REF: PG 201801144**

Municipal Director  
P.O BOX  
KILIMANJARO

24<sup>th</sup> Jan 2021

#### RE: RESEARCH CLEARANCE

The Open University of Tanzania was established by an act of Parliament No.17 of 1992, which become operational on the 1<sup>st</sup> March 1993 by public notice No. 55 in the official Gazette. The Act was however replaced by the Open University of Tanzania Charter of 2005, which became operational on 1<sup>st</sup> January 2007. In line with the Charter, the Open University mission is to generate and apply knowledge through research.

To facilitate and to simplify research process therefore, the act empowers the Vice Chancellor of the Open University of Tanzania to issue research clearance, on behalf of the Government of Tanzania and Tanzania Commission for Science and Technology, to both its staff and students who are doing research in Tanzania. With this brief background, the purpose of this letter is to introduce to you **Ms. Monica Remi Mwacha** Reg No: Pg 201801144 , pursuing Master of Art in Kiswahili We here by grant this clearance to conduct a research titled *"Tathimini za Athari za Kiusimu za Lugha ya Kibosho katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili :Mifano kutoka kwa wanafunzi wa shule za Msingi"* she will collect her data in your Municipal between 1<sup>st</sup> February 2021 to 31<sup>st</sup> March 2021

In case you need any further information, kindly do not hesitate to contact the Deputy Vice Chancellor (Academic) of the Open University of Tanzania, P.O.BOX 23409, Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820. We lastly thank you in advance for your assumed cooperation and facilitation of this research academic activity.

Yours Sincerely,

Prof. Magreth S. Bushesha  
DIRECTOR OF POSTGRADUATE STUDIES.